JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU SAYANSI NA TEKNOLOJIA

MTAALA WA ELIMUMSINGI
DARASA LA III – VI

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU SAYANSI NA TEKNOLOJIA

MTAALA WA ELIMUMSINGI
DARASA LA III – VI

© Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, 2016

Toleo la kwanza, 2016

ISBN. 978 - 9976 - 61- 434 - 3

Taasisi ya Elimu Tanzania

S.L.P 35094

Dar es Salaam.

Simu:+255 22 2773005/+255 22 277 1358

Faksi: +255 22 2774420

Baruapepe: director.general@tie.go.tz

Tovuti:www.tie.go.tz

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kutafsiri, kupiga chapa au kutoa andiko hili kwa namna yoyote ile bila idhini ya Kamishna wa Elimu, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

YALIYOMO

Orodha ya Majedwali		vii
Vifupisho		viii
Ujumbe kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu, Taasisi ya Elimu, Tanzania		xi
Dibaji		x
1.0	Utangulizi	1
1.1	Usuli	1
1.2	Muktadha wa Mtaala wa Darasa la III –VI	1
2.0	Sera na Matamko	2
2.1	Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014	2
2.2	Matamko ya Kitaifa na Kimataifa	2
3.0	Mitazamo ya Mtaala	3
3.1	Mtaala Jumuishi na unaozingatia Umahiri	3
3.2	Falsafa ya Elimu	4
3.3	Teknolojia ya Habari na Mawasiliano	4
3.4	Elimumsingi	4
3.5	Utendaji wa Mwanafunzi	5
3.6	Lugha	5
4.0	Hatua za kuandaa Mtaala	5
4.1	Hatua ya Kwanza	5
4.2	Hatua ya Pili	5
4.3	Hatua ya Tatu	6
4.4	Hatua ya Nne	6
5.0	Malengo ya Mtaala wa Elimumsingi	6
5.1	Malengo ya Elimumsingi Darasa la III –VI	6
5.2	Umahiri wa Elimumsingi Darasa la III – VI	7
5.3	Walengwa wa Mtaala wa Darasa la III – VI	7
6.0	Maeneo ya Kujifunza	7
6.1	Mgawanyiko wa Masomo kwa Darasa la III – VI	9
7.0	Umahiri wa Masomo	10
7.1	Umahiri wa Somo la Kiswahili	10
7.1.1	Mgawanyo wa Umahiri kwa Darasa la III – IV	10
7.1.2	Mgawanyo wa Umahiri kwa Darasa la V –VI	11
7.2	Competences for English Subject	12
7.2.1	Competences for English Subject Standard III	12
7.2.2	Competences for Standard IV – VI	12
7.3	Umahiri wa somo la Hisabati	13
7.3.1	Mgawanyo wa Umahiri kwa Darasa la III – IV	13

7.3.2 Mgawanyo wa Umahiri kwa Darasa la V – VI 13
7.4 Umahiri wa somo la Sayansi na Teknolojia 14
7.4.1 Mgawanyo wa Umahiri kwa Darasa la III– IV 14
7.4.2 Mgawanyo wa Umahiri kwa Darasa la V – VI 15
7.5 Umahiri wa somo la Maarifa ya Jamii 16
7.5.1 Mgawanyo wa Umahiri kwa Darasa la III – IV 16
7.5.2 Mgawanyo wa Umahiri kwa Darasa la V – VI 17
7.6. Umahiri wa somo la Stadi za Kazi 18
7.6.1 Mgawanyo wa Umahiri kwa Darasa la V– VI 18
7.7 Umahiri wa somo la Uraia na Maadili 19
7.7.1 Mgawanyo wa Umahiri kwa Darasa la III – IV 19
7.7.2 Mgawanyo wa Umahiri kwa Darasa la V – VI 20
7.8. Umahiri wa somo la Michezo na Sanaa 21
7.9 Umahiri wa somo la Elimu ya Dini 22
7.10 Compétences pour le Français Langue etrangère 22
7.10.1 La répartition de pour les niveaux III et IV 22
7.10.2 La répartition de compétences pour les niveaux V et VI 23
7.11 اللغة العربية: 24
8.0 Masuala Mtambuko 26
8.1 Umahiri unaokusudiwa kwenye Masuala Mtambuko Kulingana na Masomo Bebezi 27
9.0 Mgawanyo wa Muda wa Masomo 29
9.1 Kujifunza Somo la Elimu ya Dini 30
10.0 Kufundisha na Kujifunza 30
10.1 Utekelezaji wa Mtaala katika Madarasa Jumuishi na Madarasa Maalum 30
10.2 Shughuli za nje ya Darasa 33
10.3 Shughuli za Burudani 34
11.0 Rasilimali katika utekelezaji wa Mtaala 34
11.1 Rasilimali Watu 34
11.1.1 Mwalimu Mahiri wa Shule ya Msingi 35
11.2 Rasilimali Vitu 35
11.2.1 Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia 35
11.2.2 Samani na Majengo 36
12.0 Kupima Ujifunzaji 36
12.1 Upimaji Awali 36
12.2 Upimaji Chekeche/Gunduzi 36
12.3 Upimaji Endelezi 36
12.4 Upimaji Tamati 37
12.5 Upimaji wa Kitaifa 37

13.0 Usimamizi wa Mtaala 37
14.0 Mafunzo Endelevu ya Mtaala kwa Watekelezaji 37
15.0 Ufuatiliaji na Tathmini ya Mtaala 38
15.1 Ufuatiliaji 38
15.2 Tathmini 38
16.0 Matokeo ya Kujifunza na Viwango vya Upimaji 38
17.0 Ushiriki wa Wazazi na Jamii 45
18.0 Ubia kati ya Sekta ya Umma na Binafsi 45
Rejea..... 46

Orodha ya Majedwali

Jedwali

1. Mgawanyo wa Masomo kwa Darasa la III – IV na Darasa la V–VI. 9
2. Masomo ya kuchagua na Shughuli za nje ya Darasa III – VI. 10
3. Mgawanyo wa Umahiri kwa Darasa la III – IV Kiswahili. 10
4. Mgawanyo wa Umahiri kwa Darasa la V – VI Kiswahili. 11
5. Competences for English Standard III. 12
6. Competences for English Standard IV – VI. 12
7. Mgawanyo wa umahiri kwa Darasa la III – IV Hisabati. 13
8. Mgawanyo wa Umahiri kwa Darasa la V – VI Hisabati. 14
9. Mgawanyo wa Umahiri kwa Darasa la III – IV Sayansi na Teknolojia. 15
10. Mgawanyo wa Umahiri kwa Darasa la V – VI Sayansi na Teknolojia. 16
11. Mgawanyo wa Umahiri kwa Darasa la III – IV Maarifa ya Jamii. 17
12. Mgawanyo wa Umahiri kwa Darasa la IV– VI Maarifa ya Jamii. 18
13. Mgawanyo wa umahiri kwa Darasa la V – VI Stadi za Kazi. 19
14. Mgawanyo wa Umahiri kwa Darasa la III – IV Uraia na Maadili. 20
15. Mgawanyo wa Umahiri kwa Darasa la IV – VI Uraia na Maadili. 21
16. Umahiri wa Somo la Michezo na Sanaa III – VI. 22
17. La répartition de compétences Pour Le Francais Langue Etrangère: III – IV 23
18. La répartition de compétences Pour Le Francais Langue Etrangere: V–VI 24
19. Arabic. 25
20. Arabic. 25
21. Mgawanyo wa Masuala Mtambuka kulingana na somo bebezi na darasa linalohusika. 26
22. Umahiri wa Masuala Mtambuka kimadarasa. 27
23. Muda wa kujifunza na idadi ya vipindi kwa somo na kwa wiki. 29
24. Kufundisha na kujifunza kulingana na aina ya madarsa. 30
25. Vigezo na viwango vya upimaji. 39
26. Vigezo na Viwango vya Kupima shughuli za nje ya Darasa 44

Vifupisho

TET	Taasisi ya Elimu Tanzania
TEHAMA	Teknolojia ya Habari na Mawasiliano
WyEMU	Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi
WyEU	Wizara ya Elimu na Utamaduni
UNESCO	United Nations Educational Scientific and Cultural Organization
MMEM	Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Msingi
MKUKUTA	Mpango wa Taifa wa Kuinua Uchumi na Kupunguza Umasikini Tanzania
TEA	Tanzania Education Authority
OR-TAMISEMI	Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa
WEST	Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

Ujumbe Kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu Taasisi ya Elimu Tanzania

Mtaala huu wa Elimumsingi kwa darasa la III–VI unalenga uzoefu mpana wa kujifunza na unasisitiza mbinu za kufundisha na kujifunza ambazo zinagusa mahitaji ya kila mwanafunzi. Msisitizo upo katika kumjenga mwanafunzi katika nyanja zote za kujifunza-kiroho, kimaadili, kiakili, kimwili na kijamii. Mtaala huu umeandaliwa kwa viwango vinavyokidhi haja ya kujifunza kwa ufanisi ili kumjengea mwanafunzi umahiri wa elimumsingi kwa kuzingatia matakwa ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014. Sera hiyo inaelekeza kuwa elimumsingi ni ya lazima kwa kila mtoto wa Tanzania.

Ni suala la kujivunia kuwa na mtaala wa elimumsingi unaoakisi jitihada za serikali katika kuleta maendeleo ya kiuchumi nchini kupitia sekta ya elimu kama inavyobainishwa katika Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025. Ni matumaini yangu kwamba maudhui ya mtaala huu yatawaongoza watekelezaji kutumia fursa waliyonayo kumwezesha mwanafunzi kujenga umahiri utakaomsaidia kuyamudu maisha yake. Ili kubaini kiwango cha mafanikio katika ujifunzaji, upimaji utafanyika kwa kuzingatia uwezo wa mwanafunzi kutenda na uwezo wake katika kujipima mwenyewe.

Ninatambua kwamba tunaishi katika jamii ambayo mahitaji yake yanabadilika siku hadi siku kutokana na mabadiliko ya kisayansi, kiteknolojia na kiuchumi. Hivyo, mtaala utaendelea kuboreshwa ili kwenda sambamba na mabadiliko yanayotokea.

Mwisho ninapenda kuwashukuru wadau wa elimu kutoka taasisi mbalimbali za serikali na zisizo za serikali ambao kwa namna moja au nyingine wamefanikisha uandaaji wa mtaala huu.



Dkt. Elia Y. K. Kibga
Kaimu Mkurugenzi Mkuu
Taasisi ya Elimu Tanzania

Dibaji

Elimu bora ni kitovu cha maendeleo ya Tanzania cha kuwajengea wanafunzi umahiri unaohitajika katika ulimwengu wa mabadiliko. Ili kufikia lengo la kuwa na elimu bora, mtaala unaokidhi mahitaji ya kijamii, kitaifa na kimataifa ni muhimu. Mtaala wa Darasa la III - VI unalenga kukuza umahiri na umeandaliwa katika muundo wa masomo. Mtaala huu ni tofauti na Mtaala wa Darasa la I – II ambao umeweka mkazo katika umahiri wa Kusoma, Kuandika na Kuhesabu.

Hata hivyo umahiri wa kusoma, kuandika na kuhesabu unaendelea kupewa msisitizo katika mtaala huu kwa sababu ni msingi muhimu katika kumwezesha mwanafunzi kujifunza masomo mbalimbali kwa ufanisi. Kazi kubwa ya mwalimu ni kumwezesha mwanafunzi kujifunza na kujenga umahiri unaokusudiwa katika kila somo.Mtaala huu umetafsiriwa katika miongozo mbalimbali itakayosaidia kufafanua namna ya kufundisha masomo yaliyoainishwa katika mtaala ili kuwawezesha watumiaji kuutekeleza kama ilivyokusudiwa.

Mwongozo mkuu wa mtaala huu katika utekelezaji wa kila somo ni muhtasari ambao utatumiwa na mwalimu wakati wa kufundisha. Mwalimu hana budi kuupitia mtaala huu ili aweze kuwa na mtazamo mpana kuhusu kile anachokifundisha. Ni matarajio yangu kuwa mtaala huu utamwongoza mwalimu kufanya kazi yake kwa ufanisi. Ni muhimu pia kwa wadau wengine wa elimu kutumia mtaala huu katika kutekeleza na kufuatilia ufundishaji na ujifunzaji wa masomo yaliyoainishwa kwa ajili ya wanafunzi wa Darasa la III hadi la VI.

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia iko tayari kupokea maoni ya kuboresha mtaala huu kutoka kwa walimu na wadau wengine wa elimu. Maoni yote yapelekwe kwa Mkurugenzi Mkuu, Taasisi ya Elimu, Tanzania.

Prof. Eustella P. Bhalalusesa
Kamishna wa Elimu
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

1.0 Utangulizi

1.1 Usuli

Marekebisho ya Mtaala wa Elimu ya Msingi wa mwaka 2005 yalifanyika ili kukidhi mahitaji ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 1995, Mpango wa kisekta wa Maendeleo ya Elimu wa mwaka 1999 mpaka 2009 na Dira ya Maendeleo ya Tanzania hadi mwaka 2025. Marekebisho yalizingatia Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Msingi (MMEM) wa mwaka 2000 hadi 2006, Mpango wa Taifa wa Kuinua Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA), na mapendekezo ya tafiti anuai za kielimu, mahitaji ya kufundisha na kujifunza na maoni ya wadau wa elimu. Kabla ya mwaka 2005 mitaala kwa ngazi ya Elimu ya Awali, Msingi na Sekondari iliweka msisitizo katika maudhui ya masomo. Mtaala wa mwaka 2005 ulikuwa unajumuisha Darasa la I mpaka la VII kulingana na Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 1995. Uboreshaji ulifanyika ambapo mtaala wa mwaka 2005 ulitakiwa kuweka msisitizo katika umahiri. Hata hivyo, ilionekana kwamba mtaala ulioboreshwa bado ulikuwa umejikita zaidi katika maudhui ya masomo kuliko umahiri.

Mwaka 2015 Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, iliboresha Mtaala wa Elimumsingi kwa kuanza na Darasa la I na la II. Mtaala huu umeweka mkazo katika kukuza umahiri wa Kusoma, Kuandika na Kuhesabu. Mabadiliko hayo yametokana na ukweli wa matokeo ya tafiti mbalimbali yaliyoonesha kwamba kuna tatizo kubwa la wanafunzi kutokuwa na umahiri wa Kusoma, Kuandika na Kuhesabu. Vile vile mtaala wa mwaka 2005 kwa ngazi ya elimu ya msingi ulikamilisha mzunguko wake mwaka 2012 ambao ulikuwa ni miaka 7. Baada ya kuboresha mtaala wa Darasa la I na II, hatua iliyofuata ni kuboresha mtaala kwa Darasa la III–VI kulingana na Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014.

1.2 Muktadha wa Mtaala wa Darasa la III - VI

Mtaala huu umeandaliwa katika muktadha wa msisitizo wa Elimu kwa wote na uboreshaji wa Elimu ya Awali, Msingi na Sekondari. Msisitizo wa Elimu kwa Wote umeongeza idadi ya wanafunzi wanaojiunga na ngazi zote za elimu. Ongezeko la watoto wanaoandikishwa katika shule kunahimiza kuwa na mtaala unaokidhi mahitaji tofauti tofauti ya watoto. Maendeleo makubwa na ya haraka katika sayansi na teknolojia, na hasa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, yamesababisha kuwepo na mabadiliko makubwa katika ufundishaji na ujifunzaji na mfumo mzima wa maisha na jinsi ya kufanya kazi. Ni wazi matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano katika elimu ni jambo ambalo halikwepeki, kwani lina mahusiano makubwa na maisha ya kazi.

Kwa upande mwingine, ushiriki wa sekta binafsi katika elimu unazidi kuimarika. Hii imechangiwa na utekelezaji wa dhana ya ubia katika utoaji wa elimu nchini. Kadhalika, hii pia inaendana na mfumo wa soko huria ambao umekuza ushindani katika utoaji wa shughuli za huduma za kiuchumi na kijamii. Hivyo, kuna umuhimu kuhakikisha kuwa kuna uwiano unaofaa katika utoaji wa elimu bora. Aidha, utandawazi umechangia kuongezeka kwa ushirikiano baina ya watu na mataifa na hivyo kuweka msukumo wa kuwa na mtaala unaozingatia matakwa ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa ili kumwandaa mwanafunzi wa Tanzania kuishi katika ulimwengu wenye ushindani.

2.0 Sera na Matamko

Mtaala huu umeandaliwa kwa kuzingatia sera na matamko mbalimbali ya kitaifa na kimataifa.

2.1 Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014

Sera hii imebainisha kuwa kutakuwa na Elimumsingi ya miaka kumi yaani Darasa la Kwanza hadi la Kumi. Elimu hii itakuwa ya lazima kwa kila mtoto wa Tanzania. Baadhi ya mambo makuu yanayosisitizwa kwenye Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 ni kama ifuatavyo:

a) Umuhimu wa Kiswahili kama Lugha ya Taifa.
b) Elimu yenye viwango vya ubora unaotambulika kikanda na kimataifa na kukidhi mahitaji ya maendeleo ya Taifa.
c) Mfumo nyumbufu wa elimu.
d) Kukuza stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu.
e) Matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika kuimarisha kujifunza.
f) Ushirikiano wa wadau katika utoaji wa elimu.
g) Elimu yenye kudumisha amani.
h) Matumizi ya lugha mbalimbali katika mawasiliano.
i) Upatikanaji wa fursa sawa za elimu kwa makundi yote na
j) Elimu yenye kujenga maadili na utaifa.

2.2 Matamko ya Kitaifa na Kimataifa

Mtaala huu umezingatia matamko mbalimbali ya kitaifa na kimataifa kama ifuatavyo:

a) Mpango wa Taifa wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA). Malengo yaliyomo katika MKUKUTA yamezingatiwa katika uandaaji wa Mtaala huu. Malengo hayo ni yale yanayosisitiza kuwa na Mtaala utakaowapa walengwa maarifa, stadi na mielekeo chanya ya kushiriki vyema katika kujiletea maendeleo yao wenyewe. Hii itasaidia katika kupunguza umaskini.

b) Dira ya Maendeleo ya Tanzania hadi mwaka 2025: Dira ya Maendeleo ya Tanzania inasisitiza utoaji wa elimu bora ili kuwajengea walengwa ubunifu, ugunduzi, maarifa na stadi mbalimbali. Pia, inalenga kutoa wataalamu wenye uwezo wa kutatua matatizo ya jamii kwa kutumia sayansi na teknolojia.

c) Malengo endelevu yanalenga katika kuwa jumuishi na yenye uwiano kwa ngazi zote za elimu. Kati ya malengo 17 lengo la 4 linajihusisha moja kwa moja na elimu kama inavyoonyeshwa hapa chini.

Lengo 4: Kuhakikisha Elimu jumuishi na bora kwa wote na kukuza kujifunza. Hata hivyo malengo 17 yamefupishwa katika malengo saba (7) kama yalivyoanishwa hapo chini.

i) Kuondoa umaskini na kuboresha kilimo, usalama wa chakula na lishe.

ii) Kudumisha mifumo ya maisha ili kuimarisha afya na hali bora kwa watu wa rika zote.

iii) Kuhakikisha elimu bora inatolewa kwa watu wote.

iv) Kudumisha haki na usawa ndani ya nchi na baina ya nchi na nchi na kuboresha makazi ya watu kuwa salama, yenye amani na yaliyo katika mifumo ya haki.

v) Kuhakikisha upatikanaji wa nishati salama, maji safi na salama na usafi wa mazingira kwa watu wote.

vi) Kuimarisha ukuzaji wa uchumi, viwanda, ugunduzi, ajira, uwiano katika uzalishaji na matumizi na ujenzi wa miundombinu

vii) Kuthibiti mabadiliko ya hali ya hewa, ukuzaji bora wa mazingira, matumizi mazuri ya rasilimali za majini, mfumo wa ekolojia na hivyo kuhakikisha viumbe, wanyama na mimea kukaa pamoja kwa kutegemeana.

Kama inavyoonyeshwa katika kipengele namba 1.2 cha mtaala huu, mtaala unazingatia muktadha wa kielimu uliopo na hivyo malengo endelevu yametafsiriwa kwa kuzingatia vipaumbele vya taifa na hali halisi.

3.0 Mitazamo ya Mtaala

Uandaaji wa mtaala huu umejikita katika mitazamo mbalimbali.

3.1 Mtaala Jumuishi na Unaozingatia Umahiri

Mwelekeo wa ulimwengu unasisitiza kufundisha na kujifunza kwa kujenga umahiri na mchakato wa kujifunza unaomshirikisha mwanafunzi. Vilevile kupima ujifunzaji kwa namna endelevu kwa kumtaka mwanafunzi ajipime na kutafakari juu ya kiwango cha umahiri alichoweza kujenga. Huu ni upimaji unaomchochea mwanafunzi kujifunza zaidi. Msisitizo mwingine ni wa mwanafunzi kujengewa uwezo wa kujifunza kwa kujitegemea.

Mtaala huu umejikita katika kuhama kutoka mtaala unaosisitiza maudhui ya masomo kwenda kwenye mtaala unaosisitiza ujenzi wa umahiri ambao unajumuisha maarifa, stadi na mwelekeo. Umahiri wa kila darasa umeoneshwa na unalenga kukidhi mahitaji ya ukuaji wa mtoto na mahitaji ya kielimu. Mwanafunzi ni kitovu cha kujifunza na msisitizo upo katika kumwezesha kujifunza jinsi ya kujifunza na kujenga tabia ya kujifunza katika maisha yake yote. Wanafunzi wenye uwezo wa juu wa kutenda na vipaji watapewa fursa ya kuviendeleza na wale wenye vikwazo katika kujifunza watapata usaidizi maalum.Vile vile mtaala huu unamwezesha mwanafunzi kujifunza kwa kushiriki shughuli mbalimbali nje ya darasa kama vile michezo, sanaa, klabu za masomo na uzalishaji mali.

3.2 Falsafa ya Elimu

Mtaala huu unazingatia Falsafa ya Elimu ya Kujitegemea kama inavyoelezwa kwenye Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014. Falsafa hii imekuwa ndio msingi wa elimu Tanzania tangu mwaka 1967. Falsafa ya Elimu ya Kujitegemea inaweka msisitizo katika mambo yafuatayo:

a) Elimu inayowiana na mahitaji ya jamii au walengwa.
b) Kukuza fikra tunduizi na tabia za udadisi.
c) Kujifunza kwa kuhusisha nadharia na vitendo.
d) Kukuza kujiamini, kufanya uamuzi na kuthamini utu, na
e) Kushiriki katika shughuli za uzalishaji mali.

3.3 Teknolojia ya Habari na Mawasiliano

Matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika elimu ni jambo muhimu sana. Mtaala unaweka msisitizo katika matumizi ya teknolojia katika mchakato wa kufundisha na kujifunza. Wanafunzi wapatiwe nafasi ya kutumia teknolojia katika kujifunza masomo yote.

3.4 Elimumsingi

Mtaala huu unazingatia kwamba Elimumsingi ambayo ni ya lazima itachukua miaka 10 yaani miaka sita ya Elimu ya Msingi na minne ya Elimu ya kawaida ya Sekondari. Mwanafunzi anapomaliza hatua moja na kujiunga na nyingine huwa ni kipindi muhimu ambacho kinaweza kuwa na changamoto kwa baadhi ya wanafunzi na kuleta vikwazo katika kujifunza. Hivyo basi mtaala huu unalenga pia kuendeleza umahiri uliojengwa na mwanafunzi katika madarasa ya awali na kumwandaa kwa hatua inayofuata.

3.5 Utendaji wa Mwanafunzi

Mtaala huu umegawanyika katika hatua mbili ambazo ni darasa la III–IV na darasa la V–VI. Umahiri unaokusudiwa kujengwa kwa kila hatua umebainishwa. Hivyo, ufuatiliaji wa karibu wa utendaji wa kila mwanafunzi katika kila hatua utafanyika ili kumfanya ajenge umahiri uliokusudiwa.

3.6 Lugha

Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 inatamka kuwa lugha ya Kiswahili na Kiingereza zitatumika katika kufundishia na kujifunzia katika ngazi zote za elimu na mafunzo. Mtaala huu utatumika katika shule zinazotumia Kiswahili kama lugha ya kufundisha na kujifunza. Aidha Mtaala utakaotafsiriwa kwa Kiingereza utatumiwa na shule zinazotumia Kiingereza kama lugha ya kufundishia na kujifunza.

4.0 Hatua za Kuandaa Mtaala

Kazi ya kuboresha mtaala hupitia katika hatua mbalimbali ili kupata mtaala ambao unakidhi mahitaji ya walengwa. Katika kuandaa mtaala wa Darasa la III – VI, hatua zifuatazo zilizingatiwa:

4.1 Hatua ya Kwanza

Mikutano ya majopo ya masomo ilifanyika kwa nyakati tofauti kati ya mwaka 2010 na 2014 kwa lengo la kupata maoni ya kuboresha mtaala wa Elimu ya Msingi. Hii ilitokana na mapendekezo kuhusu mtaala wa mwaka 2005 kutoka kwa walimu, watafiti, wazazi na jamii kwa ujumla.

Katika kipindi hiki pia kulifanyika ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa mtaala wa mwaka 2005. Mrejesho uliopatikana umetumika kama kigezo cha kupitia na kuboresha mtaala huu.

4.2 Hatua ya Pili

TET ilifanya utafiti na kupata maoni kutoka kwa wadau kuhusu uboreshaji wa mtaala kwa Darasa la III – VI. Washiriki wa utafiti walikuwa walimu 300, kutoka mikoa 24 ya Tanzania Bara waliokuwa kwenye mafunzo ya Mtaala wa Darasa la I na la II katika Chuo Kikuu cha Dodoma. Wadau mbalimbali wa elimu walihojiwa. Wadau hao ni maafisa elimu wa wilaya na mikoa, wathibiti ubora wa elimu, watunga sera, viongozi wakuu wa wizara, maofisa kutoka asasi mbalimbali na wadau kutoka sekta binafsi.

4.3 Hatua ya Tatu

Hatua hii ilihusisha mkutano wa waratibu wa mitaala wa TET, ambao walipitia taarifa ya utafiti, taarifa za majopo ya masomo, mtaala wa Elimu ya Msingi wa mwaka 2005 na mtaala wa Elimumsingi Darasa la I na la II wa mwaka 2015. Pia, waratibu wa mitaala walipitia Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 na mitaala ya nchi mbalimbali za Afrika Mashariki, Afrika na nje ya Afrika. Baada ya uchambuzi huu mapendekezo ya awali ya mtaala yalitolewa. Baadaye mapendekezo hayo yaliwasilishwa kwa wadau wakuu wa elimu ambapo maoni yao yalitumika katika uandishi wa mtaala huu. Kisawidi cha kwanza cha mtaala kilipelekwa kwa wadau na kutolewa maoni. Mrejesho kutoka kwa wadau ulitumika tena kuboresha kisawidi cha mtaala.

4.4 Hatua ya Nne

Hatua hii ilihusisha mkutano wa paneli za masomo ambazo zilipitia kisawidi cha mtaala kwa kushirikiana na waratibu wa mitaala. Mrejesho kutoka katika mikutano ya paneli ulitumika tena kufanya maboresho katika maeneo mbalimbali ya mtaala. Baada ya kuingiza mapendekezo ya paneli katika kisawidi cha mtaala, utaratibu wa kuidhinishwa ulifuatwa ambapo mwenyekiti wa Baraza la Taasisi alitoa mapendekezo kwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia ya kuidhinisha mtaala huu.

5.0 Malengo ya Mtaala wa Elimumsingi

Elimumsingi inayokusudiwa kujengwa na mtaala huu ni ile inayozingatia mambo yafuatayo:

5.1 Malengo ya Elimumsingi Darasa la III hadi la VI

Elimumsingi kwa Darasa la III–VI inalenga kumjengea mwanafunzi maarifa, stadi na mwelekeo inayohitajika katika maisha ya kila siku. Yafuatayo ndiyo malengo ya Elimumsingi kwa Darasa la III–VI:

a) Kumwezesha mwanafunzi kukuza stadi za kusoma, kuandika, kuhesabu na kuwasiliana.
b) Kumwezesha mwanafunzi kuifahamu, kuitumia na kuithamini lugha ya Kiswahili.
c) Kumwezesha mwanafunzi kufahamu misingi ya utawala wa sheria.
d) Kumwezesha mwanafunzi kuthamini utamaduni wa Tanzania na wa jamii nyingine.
e) Kukuza uwezo wa mwanafunzi kufikiri, kubuni, na kutatua matatizo.
f) Kumwezesha mwanafunzi kutambua umuhimu wa maadili, uadilifu na uwajibikaji kama misingi ya raia mwema.
g) Kumwezesha mwanafunzi kushiriki katika shughuli ya michezo na sanaa pamoja na kuthamini kazi za kisanii.

h) Kumwezesha mwanafunzi kubaini na kukuza vipaji na vipawa vyake.
i) Kumwezesha kila mwanafunzi kuthamini na kupenda kufanya kazi.
j) Kumwezesha mwanafunzi kutambua, kuthamini na kutumia teknolojia na ufundi.
k) Kumwandaa mwanafunzi kwa ngazi nyingine ya elimu pamoja na kujifunza kusiko na kikomo.

5.2 Umahiri wa Elimumsingi Darasa la III hadi la VI

Umahiri wa Elimumsingi umejikita katika kumwandaa mwanafunzi wa Darasa la III hadi la VI kuwa na uwezo wa:

a) Kuwasiliana kwa ufasaha kwa lugha ya Kiswahili na Kiingereza kwa kuzungumza na kuandika.
b) Kusoma kwa kujiamini na kufahamu maandishi sahili.
c) Kutumia dhana na kanuni za kihisabati katika maisha ya kila siku.
d) Kutumia stadi za kisayansi, kiteknolojia na kiufundi katika maisha halisi ya kila siku.
e) Kuthamini utamaduni wake na wa jamii nyingine.
f) Kujali tofauti za kiimani na kiitikadi katika jamii.
g) Kushiriki katika michezo na shughuli za kisanii.
h) Kujiheshimu na kuheshimu wengine.
i) Kutenda matendo ya kizalendo.
j) Kushiriki katika kazi mbalimbali zinazoendana na umri wake.
k) Kushiriki katika shughuli zinazokuza uwezo wake wa kufikiri kimantiki na kiyakinifu.
l) Kushirikiana na wengine kwa kufanya matendo yanayokubalika katika jamii.

5.3 Walengwa wa Mtaala wa Darasa la III hadi la VI

Mtaala umebainisha makundi matatu ya wanafunzi wanaotakiwa kupatiwa elimu kama haki yao ya msingi. Kundi la kwanza ni wanafunzi wasio na ulemavu. Kundi la pili ni lile la wanafunzi wenye ulemavu waliobainishwa kwa kupitia upimaji chekeche na gunduzi kuwa wanaweza kujumuishwa katika mfumo wa madarasa ya kawaida na kuwa wanaweza kufaidika kwa kujifunza pamoja na wanafunzi wasio na ulemavu. Kundi la tatu ni lile la watoto wenye ulemavu waliobainishwa kwa upimaji chekeche na gunduzi kuwa wanahitaji mafunzo maalum ili waweze kufaidika na mafunzo. Mfumo wa mafunzo kwa watoto hawa utakuwa ni ule wa madarasa maalum au vitengo.

6.0 Maeneo ya Kujifunza

Mtaala huu una maeneo makuu sita ya kujifunza. Kila eneo la kujifunza limejengewa maarifa, stadi na mwelekeo ambao una sifa za kipekee pamoja na uhusiano na maeneo mengine ya kujifunza.

a) Lugha

Lugha ni msingi muhimu wa maendeleo ya mwanadamu na utambulisho wa utamaduni. Lugha huwezesha wanafunzi kuwasiliana katika shughuli za kila siku katika miktadha na mazingira mbalimbali. Umahiri wa lugha humwezesha pia mwanafunzi kujifunza kwa ufanisi. Msisitizo katika lugha ni kuwaandaa wanafunzi wenye umahiri wa kusikiliza, kusoma, kuzungumza na kuandika kwa ufasaha lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Pia,wanafunzi watahitajika kuwa na uelewa wa jumla wa kujieleza kwa kutumia lugha inayojumuisha alama. Vilevile, wanafunzi wanaweza kuchagua kujifunza Kifaransa au Kiarabu kwani lugha hizi zinaonekana kuwa muhimu katika biashara, uhusiano na utalii.

b) Sayansi ya Jamii

Kujifunza Sayansi ya Jamii kunalenga kuwawezesha wanafunzi kuwa na maarifa, stadi na mwelekeo utakaowawezesha kutekeleza wajibu wao katika jamii na kuchangia katika maendeleo. Eneo hili linawajengea wanafunzi uwezo wa kuelewa na kuthamini haki za binadamu na umuhimu wake, kuelewa historia ya jamii na kutekeleza wajibu wao katika jamii na nchi zilizo jirani ili wachangie katika maendeleo. Sayansi ya Jamii huwawezesha wanafunzi kuelewa, kuthamini na kuendeleza utamaduni unaofaa katika jamii pamoja na kutambua tamaduni za jamii nyingine zinazofaa. Kuelewa mazingira anamoishi, kuyatunza, kuyahifadhi na kuyatumia katika njia endelevu, kutambua na kushiriki katika kuleta mabadiliko ya kiuchumi, kijamii na kisiasa. Eneo hili la masomo ya Sayansi ya Jamii linahusisha somo la Maarifa ya Jamii na Uraia na Maadili.

c) Sayansi na Teknolojia

Sayansi na Teknolojia inahusisha maarifa na stadi za kisayansi zitakazowezesha wanafunzi kupenda na kutumia msingi ya sayansi na teknolojia katika maisha ya kila siku. Sayansi na Teknolojia inawajengea wanafunzi uwezo wa kufikiri kiyakinifu kutakaowawezesha kukabiliana na maisha ya kila siku. Kupitia sayansi mwanafunzi atajenga umahiri wa kutafuta suluhisho linaloweza kutatua matatizo katika mazingira tofauti.

d) Hisabati

Hisabati ni nyenzo muhimu katika kukuza na kuimarisha kufikiri kiyakinifu, kimantiki, kinadharia na kidhahania. Mwanafunzi atajenga uwezo wa kutumia mbinu mbalimbali katika kutatua baadhi ya matatizo anayokutana nayo katika maisha. Hii yote hufanyika katika nyanja zote za maisha na maendeleo ya binadamu. Pia, somo hili hukuza stadi zinazotumika kujifunzia masomo mengine.

e) Masomo ya Vitendo na Sanaa

Eneo hili linagusa umahiri muhimu katika maisha ya kila siku. Masomo ya eneo hili yanalenga kuwawezesha wanafunzi kupenda na kujihusisha katika kazi za mikono. Masomo haya yanawajenga kwa kuwapa stadi za awali za kufanya kazi. Kushiriki katika michezo na sanaa kunawafanya wanafunzi kujenga miili yenye afya na hasa ukizingatia mabadiliko ya mfumo wa maisha ambapo watu wengi wanazidi kutumia muda mdogo katika mazoezi ya mwili. Aidha, masomo haya yanakuza stadi za ubunifu, ushirikiano, kutatua matatizo na kukuza vipaji. Eneo hili la masomo ya vitendo linahusisha somo la Stadi za Kazi, Michezo na Sanaa.

f) Masuala ya Kiroho

Hili ni eneo linalohusika na kumwezesha mwanafunzi kukua kiroho, kukubali imani za dini na kujenga tabia ya uvumilivu na kuheshimu tofauti za kiimani na za kiitikadi wakati wote na mahali popote. Kupitia somo la Elimu ya Dini wanafunzi watajenga mwenendo unaokubalika katika jamii kwa kuimarisha uwezo wa kufikiri kiyakinifu na kutatua matatizo kwa kuzingatia misingi ya dini.

6.1 Mgawanyiko wa Masomo kwa Darasa la III hadi la VI

Wanafunzi wa Darasa la III na IV watajifunza masomo saba (7) na wanafunzi wa Darasa la V na VI watajifunza masomo nane (8) kama yanavyooneshwa katika Jedwali Na 1.

Jedwali Na 1: Mgawanyiko wa Masomo kwa Darasa la III - IV na Darasa la V - VI

Na	MASOMO YA DARASA LA III – IV	Na	MASOMO YA DARASA LA V-VI
1	Kiswahili	1	Kiswahili
2	English	2	English
3	Hisabati	3	Hisabati
4	Sayansi na Teknolojia	4	Sayansi na Teknolojia
5	Maarifa ya Jamii	5	Maarifa ya Jamii
6	Uraia na Maadili	6	Uraia na Maadili
7	Elimu ya Dini	7	Stadi za Kazi
		8	Elimu ya Dini

Kutakuwa na masomo chaguzi na shughuli za nje ya darasa. Masomo chaguzi yatafundishwa kwenye shule zenye uwezo na vifaa vya kufundishia masomo hayo. Shughuli za nje ya darasa zinahusisha klabu za masomo na maeneo mengine ya kujifunza: sanaa, michezo, kazi za uzalishaji mali na burudani, kama inavyooneshwa katika Jedwali Na 2. Ufundishaji wa Michezo na Sanaa, utafuata mwongozo elekezi ulioandaliwa na TET.

Jedwali Na. 2: Masomo ya Kuchagua na Shughuli za nje ya Darasa kwa Darasa la III-VI

Na	Masomo Kuchagua	Shughuli za Nje ya Darasa
1	Kiarabu	Klabu za Masomo na Maeneo mengine ya Kujifunza
2	Kifaransa	Michezo na Sanaa
3		Shughuli za uzalishaji mali
4		Kujisomea/Maktaba

7.0 Umahiri wa Masomo kwa Darasa la III - IV

Katika Mtaala huu kila somo limezingatia Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi.

7.1 Umahiri wa Somo la Kiswahili

Umahiri wa somo la Kiswahili umegawanywa kimadarasa kama inavyooneshwa katika jedwali namba 3 na 4.

7.1.1 Mgawanyo wa Umahiri kwa Darasa la III-IV

Ugawaji wa umahiri mkuu na umahiri mahususi katika Darasa la III-IV ni mwendelezo wa umahiri mkuu na mahususi uliojengwa kutoka Darasa la I na la II katika stadi za Kusoma na Kuandika. Jedwali Na 3. limebainisha umahiri mkuu na mahususi utakaojengwa na wanafunzi katika Somo la Kiswahili kuanzia Darasa la III – IV.

Jedwali Na. 3: Mgawanyo wa Umahiri kwa Darasa la III-IV Kiswahili

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi
1. Kuwasiliana katika miktadha mbalimbali.	1.1 Kutambua sauti mbalimbali katika matamshi ya silabi, maneno, sentensi na habari. 1.2 Kuanzisha na kuendeleza mazungumzo katika miktadha mbalimbali. 1.3 Kutumia maandishi katika mawasiliano kulingana na miktadha mbalimbali.
2. Kuonesha uelewa wa jambo alilolisikiliza au kulisoma.	2.1 Kusikiliza na kuonesha jambo alilolisikiliza. 2.2 Kusoma kwa ufasaha na kuonesha uelewa wa matini aliyosoma.

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi
3. Kutumia msamiati katika miktadha mbalimbali.	3.1 Kuzungumza kwa kuwasilisha hoja kulingana na hali mbalimbali. 3.2 Kutumia maandishi katika kuandaa matini mbalimbali. 3.3 Kusoma na kuchanganua mawazo yaliyowasilishwa katika matini mbalimbali.

7.1.2 Mgawanyo wa Umahiri kwa Darasa la V-VI

Jedwali Na. 4 limebainisha umahiri mkuu na mahususi utakaojengwa na wanafunzi katika somo la Kiswahili kuanzia Darasa la V – VI.

Jedwali Na. 4: Mgawanyo wa Umahiri kwa Darasa la V- VI Kiswahili

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi
1. Kuwasiliana katika miktadha mbalimbali.	1.1 Kuanzisha na kuendeleza mazungumzo katika miktadha mbalimbali. 1.2 Kutumia maandishi katika mawasiliano kulingana na miktadha mbalimbali.
2. Kuonesha uelewa wa jambo alilolisikiliza au kulisoma.	2.1 Kusikiliza na kuonesha uelewa wa jambo alilolisikiliza. 2.2 Kusoma kwa ufasaha na kuonesha uelewa wa matini aliyoisoma.
3. Kutumia msamiati katika miktadha mbalimbali.	3.1 Kuzungumza kwa kuwasilisha hoja kulingana na hali mbalimbali. 3.2 Kutumia maandishi katika kuandaa matini mbalimbali. 3.3 Kusoma na kuchanganua mawazo yaliyowasilishwa katika matini mbalimbali.

7.2 Competences for English language Subject

Competences for English language Subject are grouped in classes as shown in tables No. 5 and 6:

7.2.1 Competences for English Subject standard III

Table No: 5 shows competences to be developed in Standard III

Table 5: Competences for Standard III

Main Competences	Specific Competences
1. Comprehend oral and written information.	1.1 Listen and comprehend information presented orally. 1.2 Listen and comprehend phonemic symbols. 1.3 Listen, pronounce and read phonemic symbols.
2. Communicate orally and through writing.	2.1 Communicate through speaking. 2.2 Communicate through writing.
3. Acquire and use vocabulary through the four language skills (Listening, speaking, reading and writing).	3.1 Develop and use vocabulary through listening and speaking. 3.2 Develop and use vocabulary through reading. 3.3 Develop and use vocabulary through writing.

7.2.2 Competences for Standard IV-VI

Table No: 6 shows competences to be developed in Standard IV – VI

Table No: 6 Competences for Standard IV to VI

Main Competences	Specific Competences
1.Comprehend oral and written information.	1.1 Listen and comprehend information presented orally. 1.2 Read and comprehend written information.
2.Communicate orally and through writing.	2.1 Communicate through speaking. 2.2 Communicate through writing.
3. Acquire and use vocabulary through the four language skills (listening, speaking , reading and writing).	3.1 Develop and use vocabulary through listening and speaking. 3.2 Develop and use vocabulary through reading. 3.3 Develop and use vocabulary through writing.

7.3 Umahiri wa Somo la Hisabati

Umahiri wa Somo la Hisabati umegawanywa kimadarasa kama inavyoonyeshwa kwenye majedwali ya Na. 7 na Na. 8.

7.3.1 Mgawanyo wa Umahiri kwa Darasa la III-IV

Jedwali Na: 7. limebainisha umahiri mkuu na mahususi utakaojengwa na mwanafunzi katika somo la Hisabati kuanzia Darasa la III – IV.

Jedwali Na. 7: Mgawanyo wa Umahiri kwa Darasa la III-IV - Hisabati

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi
1. Kutumia lugha ya kihisabati kuwasilisha wazo au hoja.	1.1 Kutumia dhana ya namba kuwasiliana katika mazingira tofauti. 1.2 Kutumia stadi za takwimu kuwasilisha taarifa mbalimbali.
2. Kutatua matatizo katika mazingira tofauti.	2.1 Kutumia matendo ya namba ya kihisabati katika kutatua matatizo. 2.2 Kutumia stadi za uhusiano wa namba na vitu katika kutatua matatizo katika miktadha mbalimbali.
3. Kufikiri na kuhakiki katika maisha ya kila siku.	3.1 Kutumia stadi za vipimo katika miktadha mbalimbali. 3.2 Kutumia stadi za maumbo katika maisha ya kila siku. 3.3 Kutumia stadi za mpangilio kufumbua mafumbo katika maisha ya kila siku.

7.3.2 Mgawanyo wa Umahiri kwa Darasa la V – VI

Jedwali Na: 8. limebainisha umahiri mkuu na mahususi utakaojengwa na mwanafunzi katika somo la Hisabati kuanzia Darasa la V – VI.

Jedwali Na: 8. Mgawanyo wa Umahiri kwa Darasa la V - VI - Hisabati

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi
1. Kutumia lugha ya kihisabati kuwasilisha wazo au hoja.	1.1 Kutumia dhana ya namba kuwasiliana katika mazingira tofauti. 1.3 Kutumia stadi za aljebra kutatua matatizo katika maisha ya kila siku. 1.2 Kutumia stadi za takwimu kuwasilisha taarifa mbalimbali.
2. Kutatua matatizo katika mazingira tofauti.	2.1 Kutumia matendo ya namba ya kihisabati katika kutatua matatizo. 2.2 Kutumia stadi za uhusiano wa namba na vitu katika kutatua matatizo katika muktadha mbalimbali.
3. Kufikiri na kuhakiki katika maisha ya kila siku.	3.1 Kutumia stadi za vipimo katika miktadha mbalimbali. 3.2 Kutumia stadi za maumbo kufumbua mafumbo katika muktadha wa hisabati. 3.3 Kutumia stadi za mpangilio kufumbua mafumbo katika maisha ya kila siku.

7.4 Umahiri wa Somo la Sayansi na Teknolojia

Umahiri wa Somo la Sayansi na Teknolojia umegawanywa kimadarasa kama inavyooneshwa kwenye majedwali Na.9 na Na.10.

7.4.1 Mgawanyo wa Umahiri kwa Darasa la III -IV

Jedwali Na: 9. limebainisha umahiri mkuu na mahususi utakaojengwa na mwanafunzi katika somo la Sayansi na Teknolojia kuanzia Darasa la III – IV.

Jedwali Na.9: Mgawanyo wa Umahiri kwa Darasa la III – IV

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi
1. Kufanya uchunguzi na ugunduzi wa kisayansi na kiteknolojia.	1.1 Kuchunguza vitu vilivyo katika mazingira. 1.2 Kutambua aina anuai za nishati na matumizi yake. 1.3 Kutambua nadharia za kisayansi na kiteknolojia.
2. Kufahamu misingi ya Sayansi na Teknolojia	2.1 Kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA). 2.2 Kumudu stadi za kisayansi. 2.3 Kufanya majaribio ya kisayansi kwa usahihi.
3. Kutunza afya na mazingira	3.1 Kufuata kanuni za usafi ili kuwa na afya na mazingira bora. 3.2 Kufuata kanuni za afya ili kujenga afya bora. 3.3 Kutambua mifumo mbalimbali ya mwili wa binadamu.

7.4.2 Mgawanyo wa Umahiri kwa Darasa la V hadi la VI

Jedwali Na.10 limebainisha umahiri mkuu na mahususi utakaojengwa na mwanafunzi katika somo la Sayansi na Teknolojia kuanzia Darasa la V – VI.

Jedwali Na.10: Umahiri Mkuu na Mahususi kwa Darasa la V - VI

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi
1. Kufanya uchunguzi na ugunduzi wa kisayansi na kiteknolojia.	1.1 Kuchunguza vitu vilivyopo katika mazingira. 1.2 Kutambua aina anuai za nishati na matumizi yake. 1.3 Kutambua nadharia za kisayansi na kiteknolojia.
2. Kufahamu misingi ya Sayansi na Teknolojia.	2.1 Kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA). 2.2 Kumudu stadi za kisayansi. 2.3 Kufanya majaribio ya kisayansi kwa usahihi.
3. Kutunza afya na mazingira	3.1 Kufuata kanuni za usafi ili kuwa na afya na mazingira bora. 3.2 Kufuata kanuni za afya ili kujenga afya bora. 3.3 Kutambua mifumo mbalimbali ya mwili wa binadamu.

7.5 Umahiri wa Somo la Maarifa ya Jamii

Umahiri wa Somo la Maarifa ya Jamii umegawanywa kimadarasa kama inavyooneshwa kwenye majedwali ya Na 11 na Na 12.

7.5.1 Mgawanyo wa Umahiri kwa Darasa la III hadi la IV

Jedwali Na: 11 limebainisha umahiri mkuu na mahususi utakaojengwa na mwanafunzi katika somo la Maarifa ya Jamii kuanzia Darasa la III – IV.

Jedwali Na.11: Mgawanyo wa Umahiri kwa Darasa la III – IV

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi
1. Kutambua matukio yanayotokea katika mazingira yanayomzunguka.	1.1 Kutunza mazingira ya jamii inayomzunguka. 1.2 Kutumia elimu ya hali ya hewa katika shughuli za kila siku.
2. Kutambua misingi ya uzalendo katika jamii.	2.1 Kudumisha utamaduni wa Mtanzania. 2.2 Kujenga uhusiano mwema kwa jamii inayomzunguka. 2.3 Kuthamini mashujaa wetu.
3. Kutumia ramani na elimu ya anga katika maisha ya kila siku.	3.1 Kutumia ramani katika mazingira. 3.2 Kufahamu mfumo wa jua.
4. Kufuata kanuni za kiuchumi katika shughuli za uzalishaji mali.	4.1 Kuthamini na kulinda rasilimali za nchi. 4.2 Kutambua shughuli za uzalishaji mali katika jamii. 4.3 Kutumia stadi za ujasiriamali katika shughuli za kila siku.

7.5.2 Mgawanyo wa Umahiri kwa Darasa la V hadi la VI

Jedwali Na: 12 limebainisha umahiri mkuu na mahususi utakaojengwa na mwanafunzi katika somo la Maarifa ya Jamii kuanzia Darasa la V – VI.

Jedwali Na.12: Mgawanyo wa Umahiri kwa Darasa la V – VI

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi
1. Kutambua matukio yanayotokea katika mazingira yanayomzunguka.	1.1 Kutunza mazingira ya jamii inayomzunguka. 1.2 Kutunza kumbukumbu za matukio mbalimbali. 1.3 Kutumia elimu ya hali ya hewa katika shughuli za kila siku.
2. Kutambua misingi ya uzalendo katika jamii.	2.1 Kudumisha utamaduni wa Mtanzania. 2.2 Kujenga uhusiano mwema katika jamii inayomzunguka. 2.3 Kuthamini mashujaa wetu.
3. Kutumia ramani na elimu ya anga katika maisha ya kilasiku.	3.1 Kutumia ramani katika mazingira mbalimbali. 3.2 Kufahamu mfumo wa jua.
4. Kufuata kanuni za kiuchumi katika shughuli mbalimbali.	4.1 Kuthamini na kulinda rasilimali za nchi. 4.2 Kutambua shughuli za uzalishaji mali. 4.3 Kutumia stadi za ujasiriamali katika shughuli za kila siku.

7.6. Umahiri wa Somo la Stadi za Kazi

Umahiri wa Somo la Stadi za Kazi umegawanywa kimadarasa kama inavyooneshwa kwenye Jedwali Na. 13, hapo chini.

7.6.1 Mgawanyo wa Umahiri kwa Darasa la V – VI

Jedwali Na:13 limebainisha umahiri mkuu na mahususi utakaojengwa na mwanafunzi katika somo la Stadi za Kazi kuanzia Darasa la V – VI.

Jedwali Na.13. Mgawanyo wa Umahiri kwa Darasa la V- VI

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi
1. Kuwa nadhifu.	1.1 Kujenga tabia ya usafi wa mwili. 1.2 Kutunza mavazi katika kudumisha usafi. 1.3 Kutunza mazingira katika kudumisha makazi safi.
2.Kumudu mapishi mbalimbali.	2.1 Kutambua kanuni zinazohitajika katika mapishi mbalimbali. 2.2 Kutayarisha vyakula vya aina mbalimbali. 2.3 Kutengeneza vinywaji mbalimbali.
3. Kusanifu kazi za sanaa.	3.1 Kumudu misingi ya uimbaji na uigizaji. 3.2 Kutengeneza picha zenye ujumbe mbalimbali kwa jamii. 3.3 Kubuni chapa mbalimbali za sanaa za ufundi. 3.4 Kufinyanga maumbo mbalimbali. 3.5 Kutengeneza vitu kwa kutumia makunzi mbalimbali yanayopatikana katika mazingira.
4. Kufahamu stadi za ujasiriamali.	4.1 Kujenga utayari wa kujifunza. 4.2 Kutafuta masoko ya bidhaa ndogondogo. 4.3 Kutambua kanuni za usimamizi wa fedha.

7.7 Umahiri wa Somo la Uraia na Maadili

Umahiri wa Somo la Uraia na Maadili umegawanywa kimadarasa kama inavyooneshwa kwenye majedwali Na. 14 na 15.

7.7.1 Mgawanyo wa Umahiri kwa Darasa la III – IV

Jedwali Na:14 limebainisha umahiri mkuu na mahususi utakaojengwa na mwanafunzi katika somo la Uraia na Maadili kuanzia Darasa la III – IV.

Jedwali Na. 14: Mgawanyo wa Umahiri kwa Darasa la III – IV

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi
1.Kuheshimu jamii.	1.1 Kujipenda na kuwapenda watu wengine. 1.2 Kuipenda na kujivunia shule yake. 1.3 Kuipenda Tanzania kwa kuenzi tunu za nchi na asili yake.
2. Kuithamini jamii.	2.1 Kujijali na kuwajali wengine. 2.2 Kutunza mazingira na vilivyomo. 2.3 Kujenga uhusiano mzuri na watu wengine katika jamii.
3. Kuwa mwajibikaji.	3.1 Kulinda rasilimali na maslahi ya nchi. 3.2 Kusimamia majukumu yanayomhusu nyumbani na shuleni. 3.3 Kutii sheria na kanuni mbalimbali katika kutekeleza majukumu yake ya kila siku. 3.4 Kuwa na nidhamu binafsi. 3.5 Kushirikiana katika kutekeleza majukumu ya nyumbani na shuleni.
4. Kuwa mstahimilivu.	4.1 Kuvumilia katika maisha ya kila siku. 4.2 Kufikia malengo aliyojiwekea kwa kuwa na mtazamo chanya. 4.3 Kujifunza kwa kuchanganua mambo kiyakinifu.
5. Kuwa mwadilifu.	5.1 Kuaminika katika jamii. 5.2 Kutimiza majukumu yake kwa uwazi na ukweli. 5.3 Kusimamia haki.
6. Kudumisha amani.	6.1 Kuchangamana na watu wenye asili tofauti. 6.2 Kuheshimu tofauti za kiutamaduni na mitazamo miongoni mwa watu wa jamii tofauti. 6.3 Kujenga urafiki mwema na mataifa mengine.

7.7.2 Mgawanyo wa Umahiri kwa Darasa la V – VI

Jedwali Na.15 limebainisha umahiri mkuu na mahususi utakaojengwa na mwanafunzi katika somo la Uraia na Maadili kuanzia Darasa la V – VI.

Jedwali Na. 15: Mgawanyo wa Umahiri kwa Darasa la V – VI

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi
1. Kuheshimu jamii.	1.1 Kujipenda na kuwapenda watu wengine. 1.2 Kuipenda na kujivunia shule yake. 1.3 Kuipenda Tanzania kwa kuenzi tunu za nchi na asili yake.
2. Kuithamini jamii.	2.1 Kujijali na kuwajali wengine. 2.2 Kutunza mazingira na vilivyomo. 2.3 Kujenga uhusiano mzuri na watu wengine katika jamii.
3. Kuwa mwajibikaji.	3.1 Kulinda rasilimali na maslahi ya nchi. 3.2 Kusimamia majukumu yanayomhusu nyumbani na shuleni. 3.3 Kutii sheria na kanuni mbalimbali katika kutekeleza majukumu yake ya kila siku. 3.4 Kuwa na nidhamu binafsi. 3.5 Kushirikiana katika kutekeleza majukumu ya nyumbani na shuleni.
4. Kuwa mstahimilivu.	4.1 Kuvumilia katika maisha ya kila siku. 4.2 Kufikia malengo aliyojiwekea kwa kuwa na mtazamo chanya. 4.3 Kujifunza kwa kuchanganua mambo kiyakinifu.
5. Kuwa mwadilifu.	5.1 Kuaminika katika jamii. 5.2 Kutimiza majukumu yake kwa uwazi na ukweli. 5.3 Kusimamia haki.
6. Kudumisha amani.	6.1 Kuchangamana na watu wenye asili tofauti. 6.2 Kuheshimu tofauti za kiutamaduni na mitazamo miongoni mwa watu wa jamii tofauti. 6.3 Kujenga urafiki mwema na mataifa mengine.

7.8. Umahiri wa Somo la Michezo na Sanaa

Umahiri wa somo la Michezo na Sanaa umegawanywa kimadarasa kama inavyooneshwa kwenye Jedwali namba 16.

Jedwali Na. 16: Umahiri wa Somo la Michezo na Sanaa Darasa la III-VI

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi
1. Kujenga stadi za ukakamavu kwa kushiriki katika michezo mbalimbali.	1.1 Kujenga mwili wenye nguvu kwa kushiriki michezo mbalimbali. 1.2 Kujenga misuli stahimilivu katika kushiriki michezo na sanaa. 1.3 Kujenga kasi ya utendaji wa mwili katika kushiriki michezo na sanaa. 1.4 Kuwa na wepesi wa kufikiri na kufanya uamuzi sahihi wakati wa michezo.
2. Kucheza michezo na kutenda kazi za sanaa kwa ustadi.	2.1 Kuwa na hali ya ushindani katika michezo na sanaa. 2.2 Kuwa mbunifu katika kucheza na kutenda kazi za sanaa. 2.3 Kutumia stadi mbalimbali za michezo na sanaa katika kuleta burudani.

7.9 Umahiri wa Somo la Elimu ya Dini

Umahiri wa Somo la Elimu ya Dini utabainishwa na dini husika na utazingatia mahitaji ya wanafunzi wa darasa husika. Umahiri huu utatumika katika kuandaa muhtasari wa Elimu ya Dini husika kwa kushirikiana na Taasisi ya Elimu Tanzania (TET).

7.10 Compétences pour le Français Langue etrangère

Les Compétences de Français Langue Etrangère sont divisées dans les niveaux comme si dessous.

7.10.1 La répartition de pour les niveaux III et IV

Table No.17 La répartition de compétences Pour Le Francais Langue Etrangère:
III – IV

Compétences Principales	Compétences Spécifiques
1. Employer la Compréhension Orale et Ecrite dans des occasions diverses.	1.1 Utiliser des compétences acquises de l'audition pour comprendre des documents sonores et écrits dans des situations de communication diverses. 1.2 Utiliser des compétences acquises de la lecture pour lire et comprendre des textes, annonces et des messages dans des diverses situations de communication.
2. Employer la Communication dans des situations diverses.	2.1 Utiliser des compétences acquises de l'expression orale pour participer dans des conversations différentes. 2.2 Utiliser des compétences acquises de la production écrite pour rédiger des textes et des messages divers dans des situations de communication.
3. Employer le vocabulaire dans des situations différentes de communication.	3.1 Utiliser des compétences acquises de la production orale dans des conversations diverses. 3.2 Utiliser des compétences acquises de la production écrite pour rédiger des textes et messages dans de contextes divers. 3.3 Utiliser des compétences acquises de la réception écrite pour analyser des textes dans de contexte différents.

7.10.2. La répartition de compétences pour les niveaux V et VI.

Table No. 18: La répartition de compétences Pour Le Francais Langue Etrangere: V – VI

Compétences Principales	Compétences Spécifiques
1. Employer la Compréhension Orale et Ecrite dans des occasions diverses.	1.1 Utiliser des compétences acquises de l'audition pour comprendre des documents sonores et écrits dans des situations de communication diverses. 1.2 Utiliser des compétences acquises de la lecture pour lire et comprendre des textes, annonces et des messages dans des diverses situations de communication.
2. Employer la Communication dans des situations diverses.	2.1 Utiliser des compétences acquises de l'expression orale pour participer dans des conversations différentes. 2.2 Utiliser des compétences acquises de la production écrite pour rédiger des textes et des messages divers dans des situations de communication.
3. Employer le vocabulaire dans des situations différentes de communication.	3.1 Utiliser des compétences acquises de la production orale dans des conversations diverses. 3.2 Utiliser des compétences acquises de la production écrite pour rédiger des textes et messages dans de contextes divers. 3.3 Utiliser des compétences acquises de la réception écrite pour analyser des textes dans de contexte différents.

7.11. اللغة العربية:

اللغة العربية :

مهارات في الغة العربية للصف الثالث إلى الصف السادس الإبتدائي.

المهارات العامة المكتسبة بعد دراسة اللغة العربية من السنة الثالثة إلى السنة الرابعة الإبتدائي متشابهة، إلا أن هناك الإضافات لمهارات الخاصة للصف الأول والثاني الإبتدائي التي لم توضع في مكانيها الخاص لعدم وجود الصف الأول والثاني موزع بين الصفي

.الثالث والرابع الإبتدائي Jedwali No 19

	المهارات العامة	المهارات الخاصة
1.0	معرفة وفهم الخبر عن طريقة لغة الخطاب أولغة الكتابة	الأخبار عن طريقة المشافهة استماع وفهم الحروف الهجائي وعلامات الترقيم للغة العربية. - استماع ونطق وقراءة علامات الترقيم وحروف الهجائي للغة العربية.
2.0	الإتصال عن طريقة المشافهة والكتابة	**. الإتصال عن طريقة المشافهة -** **الإتصال عن طريقة الكتابة -**
3.0	استعمال المصطلحات اللغوية من خلال المهارات اللغوية الأربعة	التطوير واستعمال المصطلحات اللغوية عن طريقة الإستماع أوالحديث. - التطوير واستعمال المصلحات اللغوية عن طريقة الكتابة . - التطوير واستعمال المصطلحات اللغوية عن طريقة القراءة .

مهارات اللغة العربية للصف الرابعة إلى الصف السادسة الإبتدائي Jedwali No 20

	المهارات العامة	المهارات الخاصة
1.0	فهم لغة الحديث والكتابة	الاستماع والفهم ما يجري من الحديث باللغة العربية عن طريقة المشافهة - القراءة وفهم محتوى من الكلام
2.0	طريقة الحديث والكتابة	- الاتصال عن طريقة الحديث . الاتصال عن طريقة الكتابة -
3.0	استعمال التعبيرات اللغوية من خلال مهارات اللغوية الأربعة	اللغوية عن طريقة الاستماع والحديثسس - التطوير واستعمال مصطلحات عن طريقة القراءة . - التطوير واستعمال مصطلحات عن طريقة

8.0 Masuala Mtambuka

Masuala mtambuko ni sehemu ya maeneo ya kujifunza yanayozingatiwa katika mtaala. Masuala mtambuko yamechopekwa katika masomo mbalimbali kama masomo bebezi kulingana na ngazi ya elimu inayohusika na welewa wa mwanafunzi. Vilevile yapo masomo yatakayochopekwa masuala mtambuko wakati wa vitendo vya kufundisha na kujifunza. Masomo hayo ni pamoja na Hisabati, Kiswahili na English.

Jedwali Na. 21: Mgawanyo wa Masuala Mtambuko kulingana na Somo Bebezi na Darasa linalohusika

Na.	Suala Mtambuko	Masomo Bebezi	Darasa linalohusika	
			III – IV	V – VI
1	Elimu ya VVU na UKIMWI	• Sayansi na Teknolojia • Uraia na Maadili	√ √	√ √
2	Elimu ya usalama barabarani	Uraia na Maadili	√	√
3	Haki na wajibu wa mtoto	Uraia na Maadili	√	√
4	Elimu ya jinsia	Uraia na Maadili.	√	√
5	Stadi za maisha	• Uraia na Maadili • Stadi za Kazi	√ –	√ √
6	Elimu ya Afya ya Uzazi	Sayansi na Teknolojia	√	√
7	Elimu kuhusu rushwa	Uraia na Maadili	√	√
8	Elimu ya stadi za ujasiriamali	• Stadi za Kazi	–	√
9	Elimu ya Fedha	Stadi za Kazi	–	√
10	Elimu kuhusu dawa za kulevya	• Uraia na Maadili • Sayansi na Teknolojia	√ √	√ √
11	Elimu ya mazingira	• Maarifa ya Jamii • Sayansi na Teknolojia • Elimu ya Dini	√ √ √	√ √ √
12	Elimu ya amani	• Uraia na Maadili • Elimu ya Dini	√ √	√ √
13	Elimu ya usalama wa mitandao	• Sayansi na Teknolojia • Uraia na Maadili	√ √	√ √
14	Elimu ya utandawazi	•Sayansi na Teknolojia •Uraia na Maadili	√ √	√ √

8.1. Umahiri unaokusudiwa kwenye Masuala Mtambuko

Masuala mtambuko yanafundishwa kwa namna mbalimbali ikiwa ni pamoja na kufundishwa kwa kupitia masomo bebezi na kufundishwa kama njia na mbinu za kufundisha katika baadhi ya masomo yasiyoweza kuchopekewa maudhui ya masuala mtambuka.

Jedwali Na. 22: Umahiri wa Masuala Mtambuko Kimadarasa

Suala Mtambuko	Umahiri Kimadarasa	
	III - IV	**V- VI**
Elimu ya mazingira	a) Kusaidia kusafisha mazingira. b) Kushiriki kutunza mazingira yanayomzunguka.	a) Kusaidia kufanya mazingira kuwa ya kijani. b) Kushiriki katika shughuli za kuzuia uharibifu wa mazingira. c) Kusaidia kutunza viumbe hai . waliomo katika mazingira yake.
Elimu ya VVU na UKIMWI	a) Kutambua VVU na UKIMWI. b) Kuonyesha upendo kwa watu wanaoishi na VVU.	a) Kuchukua tahadhari, kujikinga na kuwakinga wengine na maambukizi ya VVU. b) Kujali watu wanaoishi na VVU.
Elimu ya usalama wa mtandao	Kutumia simu, luninga, redio na magazeti kwa umakini.	Kutumia kompyuta, baruapepe, na mitandao ya kijamii kwa umakini.
Elimu ya Utandawazi	Kutambua utandawazi.	Kutumia utandawazi kwa faida.
Dawa za kulevya.	Kutambua athari za matumizi ya dawa za kulevya.	Kwa kushirikiana na jamii, kutambua njia mbalimbali za kujiepusha na matumizi ya dawa za kulevya.
Elimu ya afya ya uzazi	Kutunza mwili na via vya uzazi.	a) Kutambua madhara ya ngono. b) Kujiepusha na vitendo vya ngono ili kuepuka magonjwa na mimba za utotoni.
Stadi za maisha	a) Kujitambua. b) Kujiheshimu na kuheshimu wengine.	a) Kujiamini na kufanya uamuzi sahihi mara kwa mara. b) Kushirikiana na wengine katika mambo mbalimbali. c) Kukabiliana na msongo.

Suala Mtambuko	Umahiri Kimadarasa	
	III - IV	**V- VI**
Elimu ya stadi za ujasiriamali	a) Kutumia rasilimali za nyumbani kwa njia endelevu. b) Kushiriki katika kutambua fursa za kiuchumi zinazopatikana katika mazingira yake.	a) Kutambua fursa za kiuchumi zinazomzunguka. b) Kutumia fursa za kiuchumi kujikimu.
Elimu ya fedha	a) Kutambua muundo wa fedha ya Tanzania. b) Kujenga tabia ya kutunza fedha.	a) Kutumia fedha kwa uwelevu. b) Kuhifadhi fedha kwa njia rasmi, mfano benki, kwenye simu n.k.
Elimu ya amani	a) Kutambua dhana ya amani. b) Kuepuka ugomvi.	a) Kutunza amani. b) Kutambua athari za migogoro.
Elimu ya usalama barabarani	a) Kutumia barabara kwa usahihi. b) Kutambua alama zinazomsaidia mtumiaji wa barabarani; kutumia barabara kwa usalama.	a) Kutambua alama na ishara za usalama barabarani. b) Kutunza barabara na vyombo, alama, ishara zake.
Haki na wajibu wa mtoto	a) Kutambua haki za msingi za mtoto. b) Kutambua wajibu wa mtoto.	a) Kubaini madhara ya kutowajibika kama mtoto. b) Kutambua namna ya kudai haki yake.
Elimu ya jinsia	a) Kutambua jinsi yake. b) Kutambua tofauti za jinsia.	a) Kutambua uhusiano wa kijinsia. b) Kubaini dhima ya jinsia.
Elimu kuhusu rushwa	Kutambua dhana ya rushwa.	a) Kubaini vitendo vya rushwa na madhara yake. b) Kuonyesha vitendo vya kupigana na rushwa.

9.0 Mgawanyo wa Muda wa Masomo

Mwaka wa shule utakuwa na siku **194** ambazo ni sawa na wiki **39**. Mwaka umegawanywa katika mihula miwili, hivyo kutakuwa na mihula miwili ya masomo. Kila muhula utakuwa na wiki mbili zitakazotumika kwa mitihani. Muda wa kusoma utakuwa ni saa **6** kwa siku kwa darasa la III-VI. Muda wa kipindi ni dakika **40** hivyo kufanya jumla ya vipindi **8** kwa siku isipokuwa siku ya Ijumaa ambayo itakuwa na vipindi **6** vya darasani kwa wanafunzi wote hivyo kufanya jumla ya vipindi kuwa **38** kwa wiki. Kwa shule zinazofundisha masomo ya kuchagua mwanafunzi atajifunza somo moja chaguzi na atasoma kwa vipindi 2 kwa wiki hivyo kufanya idadi ya vipindi kuwa **40** kwa wiki. Jedwali Na. **23** linafafanua muda wa kufundisha na idadi ya vipindi kwa wiki katika masomo yote yatakayofundishwa darasani na nje ya darasa.

Jedwali Na. 23 : Muda wa Kujifunza na Idadi ya Vipindi kwa Somo na kwa Wiki

		Muda wa Kujifunza na Idadi ya Vipindi kwa Wiki					
		Saa	**Dakika**	**Saa**	**Dakika**	**Idadi ya Vipindi**	
Na	**Somo Darasani**	**III-IV**		**V-VI**		**Darasa III -IV**	**Darasa V-VI**
1	Kiswahili	3	20	3	20	5	5
2	English	4	40	4	00	7	6
3	Hisabati	4	00	3	20	6	5
4	Sayansi na Teknolojia	3	20	3	20	5	5
5	Maarifa ya Jamii	2	00	2	00	3	3
6	Uraia na Maadili	3	20	3	20	5	5
7	Stadi za Kazi	-	-	1	20	-	2
8	Dini	0	40	0	40	1	1
	Jumla ya Muda wa kujifunza darasani	**21:20**		**21:20**		**32**	**32**
Masomo ya kuchagua							
9	French/ Arabic	1	20	1	20	2	2
	Jumla ya muda wa kujifunza masomo ya kuchagua	**1:20**		**1:20**		**2**	**2**
Shughuli za nje ya Darasa							
10	Klabu za masomo na maeneo mengine ya kujifunza	1:20		1:20		2	2
11	Elimu kwa Michezo na Sanaa	1:20		1:20		2	2
12	Shughuli za uzalishaji mali	0:40		0:40		1	1
13	Kujisomea/Maktaba	0:40		0:40		1	1
	Jumla ya muda wa kujifunza nje ya darasa	**4:00**		**4:00**		**6**	**6**
	Jumla ya muda wa kusoma na idadi ya vipindi kwa wiki	**25:20**		**25:20**		**38**	**38**

9.1 Kujifunza Somo la Elimu ya Dini

Wanafunzi watajifunza somo la Elimu ya Dini siku yoyote itakayopendekezwa na shule husika isipokuwa siku ya Ijumaa. Siku ya Ijumaa masomo yatafundishwa hadi saa 6 mchana, kuanzia saa 6 hadi saa 8 mchana hakutakuwa na vipindi vitakavyofundishwa kwa shule zote na kwa wanafunzi wote. Hii ni kwa sababu ya kutoa nafasi kwa wanafunzi wa madhehebu yanayoabudu siku ya Ijumaa kushiriki ibada. Wanafunzi wasioshiriki katika ibada watumie muda huo kujisomea wenyewe au kushiriki katika shughuli nyingine kwa kadiri itakavyopangwa na shule mpaka muda wa kumaliza masomo.

10.0 Kufundisha na Kujifunza

Mtaala huu umezingatia nadharia ya kujifunza ambayo inasisitiza mwanafunzi kuwa kitovu cha ujifunzaji. Kutokana na mtazamo huu jukumu la mwalimu ni kumwezesha mwanafunzi kujifunza. Kila mwanafunzi ana uwezo wa kujifunza kwa kiasi fulani hadi hapo anapohitaji msaada wa mwalimu ili ajifunze zaidi. Mtaala huu unasisitiza matumizi ya njia shirikishi katika utekelezaji wake. Katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji, mwalimu huhakikisha kuwa fursa za kutenda na kushiriki kwa wanafunzi wote ni sawa bila kujali tofauti zao. Mtazamo huu wa kufundisha na kujifunza umejikita katika falsafa ya Elimu ya Kujitegemea (EK).

10.1 Utekelezaji wa Mtaala katika Madarasa Jumuishi na Madarasa Maalum

Serikali inaweka mkazo katika kutoa elimu bora kwa wanafunzi wote wa Tanzania kupitia elimu jumuishi ambayo inatambua kuwa kila mwanafunzi anaweza kujifunza na kufanikiwa. Mtaala huu unabainisha mambo ya msingi katika kuhama kutoka katika madarasa ya kawaida kuelekea katika madarasa jumuishi na maalum. Mambo hayo ni kama yalivyofafanuliwa katika Jedwali Na. 24.

Jedwali Na. 24: Kufundisha na Kujifunza kulingana na Aina ya Madarasa

Mambo ya Kuzingatia	Madarasa Jumuishi	Madarasa Maalum/Vitengo
Idadi ya kazi za kutenda mwanafunzi	Idadi ya shughuli za kutenda wanafunzi ziwe za kutosha kulingana na uwezo wao. Hata hivyo, kwa wale wenye ulemavu shughuli za kutenda zipunguzwe kulingana na uwezo na ulemavu walionao.	Idadi ya shughuli za kutenda mwanafunzi zitaendana na mfumo wa utoaji mafunzo katika madarasa yao.
Muda wa kujifunza	Muda wa kujifunza na kujibu maswali ya upimaji utakuwa ni ule uliokubalika katika mtaala wa wanafunzi wa kawaida ila kwa wanafunzi wenye ulemavu uongezwe kulingana ulemavu na uwezo alionao.	• Muda wa kutenda shughuli mbalimbali za kujifunza kwa wanafunzi wenye ulemavu uongezwe kulingana na ulemavu na uwezo wa mwanafunzi anayehusika.

Mambo ya Kuzingatia	Madarasa Jumuishi	Madarasa Maalum/Vitengo
	• Muda wa kujibu maswali ya upimaji darasani kwa wanafunzi wenye ulemavu uongezwe. • Muda wa kumaliza mafunzo katika ngazi moja kwenda nyingine uongezwe kulingana na ulemavu na uwezo wa mwanafunzi anayehusika.	• Muda wa kutenda shughuli mbalimbali za kujifunza kwa wanafunzi wenye ulemavu uongezwe kulingana na ulemavu na uwezo wa mwanafunzi anayehusika. • Muda wa kujibu maswali ya upimaji darasani kwa wanafunzi walemavu uongezwe kulingana ulemavu na uwezo wa mwanafunzi anayehusika. • Muda wa kumaliza mafunzo katika ngazi moja kwenda nyingine uongezwe kulingana ulemavu na uwezo wa mwanafunzi anayehusika. • Muda wa kujifunza na kujibu maswali ya upimaji utaendana na mfumo wa utoaji wa mafunzo katika madarasa yao.
Kiwango cha kutoa msaada katika Kujifunza	Kila mwanafunzi apewe msaada kulingana na mahitaji yake, pia kiwango cha utoaji msaada kwa mwanafunzi mlemavu aliyejumuishwa kiongezeke kulingana na mahitaji yake.	Kiwango cha msaada unaotolewa kwa mwanafunzi kiongezeke zaidi kulingana na mahitaji yake.
Vifaa na njia/mbinu za kufundisha na kujifunza	• Vifaa na vielelezo vya aina mbalimbali vya kuona, kusikia na kugusa vitumike katika kujifunza kulingana na uwezo na ulemavu alionao.	• Vifaa na vielelezo vya aina mbalimbali vya kuona, kusikia na kugusa vitumike katika kujifunza kulingana na ulemavu walio nao.

Mambo ya Kuzingatia	Madarasa Jumuishi	Madarasa Maalum/Vitengo
	• Njia/mbinu mbalimbali shirikishi za kufundisha na kujifunza zitumike kulingana na uwezo wa mwanafunzi na pia zitumike kulingana na ulemavu walionao. • Kuwepo na programu kwa mwanafunzi mmojammoja kulingana na kiwango cha ulemavu wake.	• Njia/ mbinu mbalimbali shirikishi za kufundisha na kujifunza zitumike kulingana na ulemavu walio nao. • Kuwepo na programu ya elimu kwa mwanafunzi mmojammoja, kulingana na kiwango cha ulemavu wake.
Ushiriki wa mwanafunzi katika kujifunza	Kila mwanafunzi ashiriki katika kujifunza. Mwanafunzi mwenye ulemavu ashiriki kwa kiwango ambacho anaweza kushughulika kulingana na ulemavu alionao.	Mwanafunzi mwenye ulemavu ashiriki kwa kiwango ambacho anaweza kulingana na ulemavu alio nao.
Utatuzi wa tatizo la kujifunza	Mwanafunzi afuate kanuni zilizowekwa katika utatuzi wa matatizo wakati wa kujifunza na kutenda shughuli mbalimbali ila kwa yule mwenye ulemavu abadilishiwe kanuni zilizowekwa katika utatuzi wa tatizo, hususani kwa yale yaliyo magumu kulingana na kiwango cha ulemavu alionao.	Mwanafunzi abadilishiwe kanuni zilizowekwa katika utatuzi wa tatizo hususan kwa yale yaliyo magumu kwa kulingana na kiwango cha ulemavu alio nao.
Matarajio katika kujifunza	Matarajio yaliyopangwa/ yanayotegemewa yahimizwe ila kwa mwanafunzi mwenye ulemavu matarajio mbadala yapangwe/ yakusudiwe.	Matarajio mbadala yapangwe/ yakusudiwe kwa mwanafunzi mwenye ulemavu.
Namna ya kupata mrejesho wa kujifunza	Mwanafunzi asiye na ulemavu arejee alichojifunza kwa njia iliyobainishwa. Mwanafunzi mlemavu abadilishiwe namna ya kurejea alichojifunza kulingana na ulemavu na uwezo wake.	Mwanafunzi mlemavu abadilishiwe namna ya kurejesha alichojifunza kulingana na ulemavu na uwezo wake.

Mambo ya Kuzingatia	Madarasa Jumuishi	Madarasa Maalum/Vitengo
Uchaguzi wa Umahiri	Mwanafunzi ajifunze kilichoelekezwa ila yule mwenye ulemavu abadilishiwe kinachofundishwa kulingana na ulemavu alionao na uwezo wake.	Mwanafunzi mlemavu abadilishiwe kinachofundishwa kulingana na ulemavu na uwezo wake.
Lugha	Lugha ya kawaida itumike kwa mwanafunzi asiye na ulemavu. Lugha ya kufundishia itumike kulingana na aina ya ulemavu alionao mwanafunzi (Lugha ya alama kwa wanafunzi viziwi).	Lugha ya kufundishia itumike kulingana na aina ya ulemavu alio nao mwanafunzi (Lugha ya alama kwa wanafunzi viziwi)
Ukaaji wa darasani	Ukaaji wa darasani uwe wa kawaida unaozingatia kila mwanafunzi aweze kujifunza bila kikwazo ila kwa wale wenye ulemavu ukaaji uzingatie aina ya ulemavu alionao na ushiriki wake katika kujifunza na wenzake wasio na ulemavu.	Ukaaji wa darasani kwa mwanafunzi mwenye ulemavu uzingatie aina ya ulemavu alio nao na ushiriki wake katika kujifunza.
Usalama	Usalama wa kila mwanafunzi uzingatiwe, hususani ule wa mwenye ulemavu wa ngozi (Albino).	Usalama wa kila mwanafunzi uzingatiwe kulingana na hali ya ulemavu alionao na hasa mwenye ulemavu wa ngozi (Albino).

10.2 Shughuli za Nje ya Darasa

Hizi ni kazi zitakazofanyika kwa lengo la kuimarisha maarifa na stadi ambazo mwanafunzi amejifunza ndani ya darasa. Hii itamsadia mwanafunzi kuchangamana na watu wengine pamoja na mazingira ya nje ya darasa, hivyo kuleta ujenzi wa maana kwa yale anayojifunza. Shughuli hizo zitajumuisha klabu za masomo na maeneo mengine ya kujifunza, shughuli za michezo na uzalishaji mali, shughuli za utamaduni na shughuli za malezi na unasihi ambazo zitawasaidia wanafunzi kuweza kujifunza kwa kina.

a) Klabu za Masomo na Maeneo Mengine ya Kujifunza

Klabu hizi zitahusisha masomo mbalimbali pia zitahusisha klabu za Masuala Mtambuka kama vile Klabu ya mazingira, VVU na UKIMWI, Jinsia, Haki za mtoto, Stadi za maisha, kupinga/kudhibiti rushwa, afya, uelimishaji rika, biashara na usalama barabarani.

b) Shughuli za Michezo na Sanaa

Shughuli hizi zitawawezesha wanafunzi kuibua vipaji na vipawa ambavyo vitapaswa kuendelezwa. Michezo itafanyika kwa wanafunzi wote kufuatana na ratiba itakayopangwa na shule husika. Michezo hiyo ni pamoja na: uigizaji, uimbaji, riadha, mpira wa miguu, mikono, kikapu, wavu, meza, mchezo wa bao na michezo mingine.

c) Shughuli za Uzalishaji Mali

Shughuli hizi zitajumuisha shughuli mbalimbali za uzalishaji mali shuleni ambazo ni pamoja na duka la shule, bustani za mboga na maua, ufugaji, kilimo, uchongaji, uchoraji na biashara ndogondogo pamoja na kubuni vitega uchumi vya shule.

10.3 Shughuli za Burudani

Shughuli za burudani na matamasha zitafanyika mara moja kwa muhula. Kila shule itaainisha na itapanga shughuli mbalimbali zitakazowashirikisha wanafunzi wote wakiwemo wenye mahitaji maalum ili kuleta usawa kwa kila mwanafunzi kuburudika. Tuzo zitatolewa kwa wanafunzi watakaofanya vizuri ili kuwatia moyo wa kuendeleza zaidi vipaji vyao.

Burudani ni shughuli anazofanya mtoto zinazoburudisha mwili na akili nje ya darasa au baada ya masomo. Shughuli hizi humpa mtoto nguvu na maarifa ya kuendelea kujifunza vizuri masomo mengine ya kitaaluma. Katika kuendeleza burudani shuleni, mtaala huu umelenga kufanya yafuatayo:

a) Kuibua vipaji na ubunifu.
b) Kuendeleza vipaji kama vile kuigiza, dansi, kuimba, ufundi, michezo na kutengeneza vitu mbalimbali vya ubunifu.
c) Kuondoa msongo wa mawazo kwa njia ya burudani.
d) Kuwapa wanafunzi nafasi ya kuburudika kwa kuona vitu mbalimbali kwa kufanya ziara katika maeneo ya utalii na kihistoria.
e) Kujifunza mambo kwa vitendo.

Katika kusimamia burudani shuleni, walimu na wanafunzi wenye mwelekeo katika fani mbalimbali watasaidiana na wataalamu katika usimamizi wa shughuli za burudani.

11.0 Rasilimali katika Utekelezaji wa Mtaala

Viwango vya rasilimali katika utekelezaji wa mtaala vimegawanywa katika makundi mawili. Makundi hayo ni rasilimali watu na rasilimali vitu.

11.1 Rasilimali Watu

Rasilimali watu ni nguzo muhimu katika kutekeleza mtaala ili kufanikisha shughuli za kujifunza shuleni. Rasilimali watu inajumuisha:

11.1.1 Mwalimu Mahiri wa Shule ya Msingi

Mwalimu wa Shule ya Msingi atakua yule ambaye amepata mafunzo ya kufundisha ngazi hii ya elimu. Sifa za mwalimu wa shule ya msingi zimefafanuliwa katika kiunzi cha umahiri wa mwalimu. Sifa hizo ni kama zifuatazo:

a) Kufundisha

Anatakiwa kuwa na stadi na maarifa ya:

i) Kuandaa somo linalolenga kukuza umahiri wa mwanafunzi.
ii) Kuhusianisha stadi mbalimbali.
iii) Kufundisha wanafunzi wenye uwezo tofauti.
iv) Kutumia teknolojia ya habari na mawasiliano katika kufundisha.

b) Kupima na Kufanya Tathmini

Awe na maarifa na stadi za:

i) Kuandaa zana za upimaji kwa kila somo.
ii) Kutumia njia zinazofaa kuwapima mwanafunzi.
iii) Kutunza kumbukumbu za maendeleo ya mwanafunzi.
iv) Kutoa mrejesho kwa mwanafunzi na wazazi utakaoboresha ujifunzaji.

11.2 Rasilimali Vitu

Rasilimali vitu itajumuisha vitu vifuatavyo:

11.2.1 Vifaa vya Kufundisha na Kujifunza

Mihtasari, miongozo, vitabu, na zana za kufundishia na kujifunzia ni vya muhimu katika utekelezaji wa mtaala wa Elimumsingi ili kukidhi malengo ya elimu yanayotarajiwa. Vitabu vya kiada na ziada vitakavyotumika ni vile vilivyopendekezwa na kupitishwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inayosimamia uthibiti wa vifaa vya kielimu. Mihtasari na miongozo ya masomo itakayotumika ni ile itakayoandaliwa na TET na kuidhinishwa na wizara inayohusika na elimu. Kufundisha na kujifunza kutafanikiwa ikiwa vifaa vya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano na matumizi yake vitazingatiwa. Kila shule inatakiwa kuwa na vifaa na vitendea kazi za shughuli za michezo, sanaa na fani mbalimbali.

Kwa wanafunzi wenye ulemavu, vifaa na vielelezo vya aina mbalimbali (kuona, kusikia na kugusa) vitumike katika kujifunza kulingana na ulemavu alio nao mwanafunzi.Kuwepo na mashine za breli kwa wenye ulemavu wa kuona na vikuza sauti kwa wenye ulemavu wa kusikia.

11.2.2 Samani na Majengo

Samani na majengo yazingatie walengwa wa aina zote wakiwemo wasichana, wavulana na wote wenye mahitaji maalum. Madarasa na majengo mengine kama vile maktaba yajengwe kwa kuzingatia viwango vilivyowekwa na wizara inayohusika na elimu. Samani na majengo ya shule kama vile ngazi na vyoo viwe rafiki kwa matumizi ya mwanafunzi mwenye ulemavu.

12.0 Kupima Ujifunzaji

Upimaji ni sehemu muhimu katika tendo la kufundisha na kujifunza. Kupima kutamwezesha mwalimu kubaini kufikiwa kwa ujenzi wa umahiri uliokusudiwa. Kupima kutafanyika kwa kutumia zana mbalimbali zikiwemo mitihani ya kuandika, uchunguzi makini, mahojiano, maswali ya ana kwa ana, mkoba wa kazi na orodha hakiki. Upimaji wa maendeleo ya mwanafunzi utahusisha upimaji endelevu na tamati. Upimaji tamati utahusisha pia upimaji wa kitaifa ambao utafanyika kwa Darasa la IV na VI.

12.1 Upimaji Awali

Upimaji huu unafanyika kabla ya mafunzo ili kupima kiwango cha uelewa na umahiri wa mwanafunzi kumwezesha mwalimu kujua umahiri alio nao mwanafunzi kabla ya mafunzo rasmi.

12.2 Upimaji Chekeche/Gunduzi

Upimaji huu ni sehemu ya upimaji endelevu ambapo unafanyika ili kupata taarifa kuhusu uwezo wa mwanafunzi katika kumudu stadi mbalimbali. Taarifa hizi zitumike katika kutoa ushauri na msaada stahiki. Wakati fulani msaada wa mtaalamu wa afya unaweza kuhitajika hasa kwa watoto wenye ulemavu.

Pamoja na upimaji gunduzi, upimaji chekeche utatumika ili kubaini wanafunzi wenye vikwazo katika kujifunza ili kuandaa mipango ya kuwasaidia. Aina hii ya upimaji inaweza kufanyika baada ya mwanafunzi kujifunza kwa miezi mitatu na kuendelea.

12.3 Upimaji Endelezi

Upimaji huu utafanyika wakati wote wa tendo la kufundisha na kujifunza ili kutoa mrejesho kwa mwalimu na mwanafunzi. Mrejesho utamsaidia mwanafunzi kuelewa maeneo yenye ugumu ambayo yanahitaji kutiliwa mkazo, pia utamsaidia mwalimu kubaini wanafunzi wenye matatizo ya ujifunzaji ili aweze kusaidiwa. Zana za upimaji zitakazotumika ni pamoja na uchunguzi makini, mahojiano, mazoezi, maswali ya ana kwa ana, mkoba wa kazi. Upimaji huu pia, utatumika kubaini vipaji mbalimali vya mwanafunzi kama ubunifu, uchoraji, sanaa, michezo na tabia.

12.4 Upimaji Tamati

Upimaji huu utahusisha mitihani ambayo itafanyika mwisho wa kila mwezi, muhula na mtihani wa mwisho utakaotumika kama kigezo cha mwanafunzi kutoka hatua/ngazi moja kwenda ngazi nyingine. Upimaji huu utahusisha mtihani wa kuandika, maswali ya ana kwa ana na uchunguzi makini.

12.5 Upimaji wa Kitaifa

Kutakuwa na upimaji wa kitaifa kwa Darasa la IV na VI. Mwanafunzi atapimwa ili kubaini kama umahiri unaotarajiwa umefikiwa ili avuke ngazi moja kwenda nyingine (yaani kutoka Darasa la IV kwenda la V na kutoka Darasa la VI kwenda kidato cha I). Upimaji huu hautakuwa wa mchujo bali utatumika kubaini upungufu wa ujifunzaji alionao mwanafunzi ili asaidiwe kabla hajaingia ngazi ya juu. Upimaji huu utahusisha mtihani wa kuandika, maswali ya ana kwa ana na uchunguzi makini.

Upimaji wa kitaifa katika Darasa la IV na VI utaandaliwa kitaifa na Baraza la Mitihani la Tanzania. Zana za upimaji zitasambazwa katika shule na usahihishaji utafanyika katika ngazi ya shule. Ratiba ya upimaji itakuwa moja kwa nchi nzima. Matokeo ya upimaji yatatumika katika shule husika ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji. Matokeo yatawasilishwa Baraza la Mitihani ambalo litatoa matokeo ya nchi nzima.

13.0 Usimamizi wa Mtaala

Usimamizi wa mitaala ni jambo muhimu katika kuhakikisha unatelekezwa kama ulivyokusudia. Usimamizi wa utekelezaji wa mtaala utafanyika kuanzia ngazi ya shule hadi wizara. Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaala ni msimamizi mkuu wa utekelezaji wa mtaala huu kupitia idara yake ya elimu. Usimamizi katika ngazi ya shule ni nguzo kuu katika utekelezji wa mtaala, Walimu wakuu, Kamati za Shule na Maafisa Elimu Kata watakuwa ndio wasimamizi wakuu katika ngazi ya shule. Hivyo kwa kupitia vikao watajadili maendeleo ya utekelezaji wa mtaala. Wasimamizi wengine wa mtaala ni Wakurugenzi wa Manispaa au Halmashauri kupitia Maafisa Elimu Wilaya katika ngazi ya wilaya na pia Maafisa Elimu Mkoa watasimamia utekelezaji wa mtaala katika ngazi ya mkoa. Kwa ujumla usimamizi wa mtaala huu unaendana na ugatuaji wa baadhi ya majukumu ya elimu kutoka serikali kuu kwenda serikali za mitaa.

14.0 Mafunzo Endelevu ya Mtaala kwa Watekelezaji

Walimu, wasimamizi, wadhibiti ubora pamoja na wadau wengine wa mtaala, watapatiwa mafunzo yatakayowawezesha kutekeleza mtaala huu kwa ufanisi. Taasisi ya Elimu Tanzania itandaa mafunzo ya mtaala kwa walimu kazini na wadau wengine. Mafunzo haya yatatolewa kwa njia ya ana kwa ana na masafa. Vyuo vya ualimu na vyuo vikuu vinavyoandaa walimu wa ngazi hii ya elimu vitakuwa na jukumu la kufundisha walimu tarajali kuhusu mtaala huu.

15.0 Ufuatiliaji na Tathmini ya Mtaala

Ufuatiliaji na tathmini ya mtaala utafanyika kwa kuzingatia mwongozo wa taifa wa ufuatiliaji na tathmini uliondaliwa na WyEMU.

15.1 Ufuatiliaji

Ufuatilaji wa utekelezaji wa mtaala unalenga kukusanya taarifa kuhusu ufanisi wa mtaala. Wadau wote wakuu wa Elimu watahusika katika kufuatilia utekelezaji wa mtaala kama kamati za shule, walimu, wazazi, wanafunzi na wathibiti ubora. Wafuatiliaji hawa wamegawanyika katika makundi mawili: wafuatiliaji wa ndani na wa nje. Walimu wakuu ni wafuatiliaji wa ndani na wa mwanzo wa utekelezaji wa mtaala. Mwongozo wa ufuatiliaji wa wizara inayohusika na elimu unatoa maelezo ya majukumu ya kila mdau katika kuhakikisha mtaala unatekelezwa kwa ufanisi. Taarifa za ufuatiliaji zitachambuliwa na kupelekwa TET na kwa wadau wengine wakuu wa elimu ambapo zitatumika katika mikakati ya kuimarisha utekelezaji wa mtaala.

15.2 Tathmini

Tathmini ya mtaala inalenga kubaini maeneo yanayohitaji kuboreshwa. Tathmini huangalia mambo yote yaliyo katika mtaala ikiwemo malengo yaliyokusudiwa, maudhui, njia za kufundishia na kujifunzia, upatikanaji wa vifaa na zana za upimaji wa maendeleo ya wanafunzi, uwezo wa walimu katika kufundisha na mazingira ya kufundishia na kujifunzia. Tathmini endelezi na tamati za mtaala zitafanyika kwa kuhusisha wadau mbalimbali wakiongozwa na TET. Tathmini tamati itafanyika kila baada ya miaka minne wakati tathmini endelezi itafanyika muda wote wa ufundishaji na ujifunzaji.

16.0 Matokeo ya Kujifunza na Viwango vya Upimaji

Mafanikio ya utekelezaji wa mitaala yatapimwa kwa kuangalia kiwango cha kutenda cha mwanafunzi. Vigezo na viwango vya kupima utendaji vitakavyozingatiwa kimasomo vimeainishwa katika Jedwali Na.25.

Jedwali Na. 25 : Vigezo na Viwango vya Upimaji

Somo	Vigezo vya Upimaji	Upimaji wa Utendaji
Kiswahili	1. Kuwasiliana katika miktadha mbalimbali.	Mwanafunzi atapimwa uwezo wake katika kutambua sauti katika matamshi ya silabi, maneno na herufi mwambatano, kutumia lugha ya mazungumzo katika miktadha mbalimbali na kutumia maandishi katika mawasiliano kulingana na miktadha mbalimbali.
	2. Kusoma na kufahamu katika kujenga uwezo wa kujieleza kwa namna mbalimbali.	1. Mwanafunzi atapimwa uwezo wake katika kusikiliza na kumudu mazungumzo. 2. Kusoma maandiko mbalimbali kwa ufasaha kwa kuzingatia kanuni za uandishi.
	3. Kutumia msamiati katika miktadha mbalimbali.	1. Mwanafunzi atapimwa uwezo wake katika kuzungumza kwa kuwasilisha hoja kulingana na hali mbalimbali. 2. Kutumia maandishi katika kuandaa matini mbalimbali na kusoma katika kuchanganua mawazo yaliyowasilishwa kwenye matini mbalimbali.
English	1. Comprehend oral and written information.	1. A pupil will be assessed on his /her ability to comprehend information presented orally. 2. A pupil will also be assessed on his /her ability to pronounce phonemic symbols.

Somo	Vigezo vya Upimaji	Upimaji wa Utendaji
	2. Communicate orally and through writing.	A pupil will be assessed on his /her ability to communicate through speaking and writing.
	3. Acquire and use vocabulary through the four language skills (Listening, speaking, reading and writing).	A pupil will be assessed on his/her ability to develop and use speaking, reading and writing skills.
Hisabati	1. Kujenga stadi za kufikiri na kuhakiki katika maisha ya kila siku.	Mwanafunzi atapimwa uwezo wake wa kutumia stadi za vipimo, maumbo na mafumbo katika miktadha mbalimbali.
	2. Kutumia Hisabati kutatua matatizo katika mazingira tofauti	Mwanafunzi atapimwa uwezo wake wa kutumia matendo ya namba na uhusiano wa namba na vitu kutatua matatizo katika miktadha mbalimbali
	3. Kutumia lugha ya kihisabati katika kuwasilisha wazo au hoja.	Mwanfunzi atapimwa uwezo wake wa kutumia dhana ya namba na takwimu kuwasilisha wazo au hoja katika miktadha mbalimbali.
Sayansi na Teknolojia	1. Kumudu stadi za uchunguzi wa kisayansi na kiteknolojia katika maisha ya kila siku.	Mwanafunzi atapimwa uwezo wake katika kutumia nadharia za kisayansi kukuza matumizi ya stadi za uchunguzi katika mazingira yake.
	2. Kutumia stadi za kisayansi na kiteknolojia katika maisha ya kila siku.	Mwanafunzi atapimwa uwezo wake katika kutumia maarifa na stadi za kisayansi na kiteknolojia katika kutatua matatizo mbalimbali.

Somo	Vigezo vya Upimaji	Upimaji wa Utendaji
	3. Kumudu stadi za usafi wa mwili na utunzaji wa mazingira.	Mwanafunzi atapimwa uwezo wake katika kumudu kanuni za afya na kutunza mazingira katika maisha ya kila siku.
Maarifa ya Jamii	1. Kujenga uzalendo.	Mwanafunzi atapimwa uwezo wake katika kujenga uhusiano mwema katika jamii, kuthamini utamaduni wake na kuwaenzi mashujaa wa Tanzania na Afrika kwa ujumla.
	2. Kumudu stadi za ugunduzi na kubashiri mabadiliko mbalimbali katika mazingira.	Mwanafunzi atapimwa uwezo wake katika kutumia ramani, kuelezea sura ya nchi na maliasili zake pamoja na kugundua mabadiliko yanayoweza kutokea katika uso wa dunia kwa kutumia elimu ya mfumo wa jua.
	3. Kusimamia shughuli mbalimbali za kiuchumi katika jamii na taifa.	Mwanafunzi atapimwa uwezo wake katika kutambua shughuli za uzalishaji mali, kutumia stadi za ujasiriamali na kuthamini rasilimali za nchi kwa maendeleo ya Taifa.
	4. Kutabiri matukio na kuchukua tahadhari	Mwanafunzi atapimwa uwezo wake katika kutunza kumbukumbu, mazingira na kupanga shughuli mbalimbali kulingana na hali ya hewa ya nchi yake.
Uraia na Maadili	1. Kuheshimu jamii.	Mwanafunzi atapimwa kiwango cha uwezo wake wa kujipenda mwenyewe, kuwapenda watu wengine, kuipenda na kujivunia shule yake pamoja na kuipenda nchi yake kwa kuzienzi tunu za nchi na asili yake.

Somo	Vigezo vya Upimaji	Upimaji wa Utendaji
	2. Kuthamini jamii.	Mwanafunzi atapimwa uwezo wake wa kujijali na kuwajali wengine, kutunza mazingira na vilivyomo kujenga uhusiano mwema na watu wengine.
	3. Kuwa mwajibikaji.	Mwanafunzi atapimwa uwezo wake katika kulinda rasilimali na maslahi ya nchi, kusimamia majukumu, kutii sheria na kanuni, kuwa na nidhamu binafsi, na kuwa na ushirikiano na wenzake katika kutekeleza majukumu mbalimbali.
	4. Kuwa mstahimilivu.	Mwanafunzi atapimwa kiwango chake cha kuvumilia katika maisha, kufikia malengo aliyojiwekea kwa kuwa na mtazamo chanya na kujifunza kwa kuchanganua mambo kiyakinifu.
	5. Kuwa mwadilifu.	Mwanafunzi atapimwa kiwango chake cha kuaminika katika jamii, kusimamia haki na kutimiza majukumu mbalimbali kwa uwazi na ukweli.
	6. Kudumisha amani.	Mwanafunzi atapimwa uwezo wake wa kuchangamana na watu wenye asili tofauti, kutambua tofauti za kiutamaduni na mitazamo katika jamii na kujenga urafiki mwema na mataifa mengine.

Somo	Vigezo vya Upimaji	Upimaji wa Utendaji
French	1. Comprendre à l'oral et à l'écrit des informations dans des occasions diverses. 2. S'exprimer à l'oral et à l'écrit dans des situations diverses	L'apprenant sera évalué sous la base de compréhension des diverses documents sonores et écrits. L'apprenant sera évalué sous la base de s'exprimer à l'oral et à l'écrit dans des situations diverses.
	3. Produire à l'oral et à l'écrit en utilisant le vocabulaire acquis dans des situations différentes.	L'apprenant sera évalué sous la base de produire à l'oral et à l'écrit en utilisant le vocabulaire acquis dans des situations différentes.

.الجدول رقم : 28 المواضيع التي تقاس من المادة وكيفية قياستها

المادة	المقياس المنظور به في عملية التقويم	قياس الكم المحصول في الدراسة
اللغة العربية	الاتصالات في المقتضيات المختلفة -	يمتحن الطالب قدرته على التمييز بين الأصوات المختلفة عند النطق بالحروف ، الكلمات ، والحروف عند اتصالها ، استعمال لغة المشاف هة في مقتضيات مختلفة ، مع استعمال الكتابة في الاتصالات متماشيا مع مقتضيات . مختلفة
	القراة والفهم في بناءقدرات على تعريف - .نفسه بأسلوب مختلفة	يمتحن الطالب قدرته على الاستماع - . والقدرة على التحدث قراءة والكتابات المختلفة مع - .مراعات القوانين في الكتابة
	استعمال مصطلحات اللغة في المقتضيات .المختلفة	يمتحن الطالب قدرته على استماع والتحدث باللغة العربية وطرح المضوع في أحوال . مختلفة استعمال كتابات مختلفة في استعداد متون - مختلفة مع القراءة لمعرفة أفكار مختلفة في هذه المتون

Vigezo na viwango vya kupima utendaji vitakavyozingatiwa kwa shughuli za nje ya darasa vimeainishwa katika Jedwali Na.26.

Jedwali Na. 26 Vigezo na Viwango vya Kupima Shughuli za nje ya Darasa

Somo	Vigezo vya Upimaji	Upimaji wa Utendaji
Michezo na Sanaa	1. Kujenga stadi za ukakamavu kwa kushiriki katika michezo mbalimbali.	Mwanafunzi atapimwa katika kushiriki michezo, kuwa mvumilivu na kufanya uamuzi katika shughuli za michezo na sanaa.
	2.Kucheza michezo na kutenda kazi za sanaa kwa ustadi	Mwanafunzi atapimwa katika ushindani wa michezo na sanaa, nidhamu, ushirikiano na uthubutu katika michezo na sanaa.
Klabu za Masomo na maeneo mengine ya kujifunza	1. Kuunda klabu za masomo na maeneo mengine ya kujifunza.	Mwanafunzi atapimwa uwezo wake katika kuunda, kusimamia na kuongoza klabu za somo linalohusika.
	2. Kushiriki shughuli za klabu za masomo na maeneo mengine ya kujifunza.	Mwanafunzi atapimwa uwezo wake katika kubuni na kushiriki shughuli mbalimbali za klabu za masomo.
Shughuli za uzalishaji mali	1. Kubuni shughuli mbalimbali za kuzalisha mali.	Mwanafunzi atapimwa uwezo wake katika kubuni na kushiriki katika shughuli mbalimbali za kuzalisha mali shuleni na nyumbani.
	2. Kufanya na kusimamia shughuli za kuzalisha mali.	Mwanafunzi atapimwa uwezo wake katika kusimamia na kupata faida kwenye shughuli za uzalishaji mali.

17.0 Ushiriki wa Wazazi na Jamii

Malezi na maendeleo ya mtoto huanzia katika ngazi ya familia, ikisaidiana na jamii inayomzunguka. Ushiriki wa wazazi na jamii katika kuboresha Elimu ni jambo muhimu kwa malezi ya mwanafunzi, hususan ushiriki wao katika kufuatilia maendeleo ya wanafunzi kitaaluma, kitabia, kiustawi na kuwasaidia kujifunza. Vile vile kushiriki katika ujenzi wa miundombinu ya shule.

18.0 Ubia kati ya Sekta ya Umma na Binafsi

Sekta ya Elimu na Mafunzo ni eneo muhimu la uwekezaji kwa njia ya ushirikiano baina ya sekta ya umma na binafsi. Lengo kuu ni kuongeza uwezo wa sekta ya Elimu na Mafunzo katika kupanua na kuimarisha miundombinu wezeshi, taaluma, utaalamu na huduma mbalimbali katika ngazi zote za elimu na mafunzo. Serikali imeweka utaratibu wa ubia kati yake na sekta binafsi katika utekelezaji wa Elimu ya Msingi. Ushiriki wa sekta binafsi katika kuendeleza elimu, utajumuisha mambo mbalimbali yakiwemo;

a) Kuchangia gharama za mafunzo kwa walimu wakati wa mafunzo elekezi.
b) Ujenzi wa madarasa, vyoo na maktaba.
c) Kusaidia Wizara ya Elimu kutoa elimu kwa watoto wa Tanzania.
d) Kutoa vifaa vya kufundishia na kujifunzia.

Rejea

Bajumuzi J. (2002).*Performance of the Visually Impaired Pupils in Tanzania*. Dar es Salaam. (Unpublished Document).

Barnes, D (1982). *Practical Curriculum Study. London*: Routledge and Kegan Paul: East Africa Cummunity, (2013). *Draft Harmonised Curriculum Structures and Framework for East Africa Community. Primary Education for East Africa.* Institute of Curriculum Development (ICD), (1990). *A Summary Report on Baseline Survey* o*n Primary, Secondary and Teacher Education Curriculum Reform inTanzania Mainland*. Dar es Salaam. (Unpublished Document).

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, (2014). *Sera ya Elimu na Mafunzo. Dar – es- Salaam*: WyEMU

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, (1998). *Waraka wa Elimu Namba 5 wa Somo la Dini. Dar – es- Salaam:* WyEU

Ministry of Education and Culture (MOEC), (1995). *Education and Training Policy. Dar-Es- Salaam*:WyEU

MOEC. (2001). *A Baseline Survey on Knowledge, Attitudes and Practices (KAP) in Tanzania Mainland*. Dar es Salaam:UNFPA

Njabili F. A. (1993). *Practical Guide for Classroom Measurement and Testing. The Basic Essentials.Dar es Salaam*: Mture Publishers

Morsh C. J. (1977). *Planning Management and Ideology: Key Concepts for Undestanding Curriculum.* UK: Falmer Press

Taasisi ya Elimu Tanzania (TET), (2004). *Ripoti ya Utafiti wa Kuboresha Mtaala wa Elimu ya Msingi.* Dar es Salaam (Kisawidi: Rekebisho la Kwanza); Agosti 2004.

Taasisi ya Elimu Tanzania (TET), (1999).*Ripoti ya Ufuatiliaji wa Muundo Mpya wa Masomo katika Shule za Msingi Tanzania Bara*.Dar es Salaam. (Andiko Lisilochapishwa).

Taasisi ya Elimu Tanzania (TET), (2003).*Ripoti ya Warsha ya Kudurusu Mada za Elimu Dhidi ya Ukimwi katika Masomo Chukuzi kwa Shule za Msingi na Sekondari*. TET, Dar Es Salaam.

Taasisi ya Elimu Tanzania (TET), (2004).NCDF: A *Guide to Innovative Teaching and Learning. Dar es Salaam*. (Unpulished Document).
Tanzania Institute of Education. (TIE), (2004).*National Curriculum Development Framework (NCDF): Core Document*. Dar es Salaam. (Unpublished Document)
Tanzania Institute of Education (TIE), (2004). NCDF. *A Guide to Assessment and Examination. Dar es Salaam*, (Unpublished Document).

Tanzania Institute of Education (TIE). (2004).NCDF. *A Curriculum Guide to Primary Education*. Dar es Salaam. (Unpublished Document).

Tanzania Institute of Education (TIE), (2014).*Report of the Workshop for Curriculum Implementers and Supervisors on the Review of Pre-primary and Primary Curriculum* (unpublished Document).

Tanzania Institute of Education (TIE), (2014). *Report of the Workshop for Policy Makers and Curriculum Implementers on the Review of Pre-primary and Primary Curriculum* (unpublished Document).

Tanzania Institute of Education (TIE), (2014).*Report of the Workshop on critical analysis of Pre-primary and Primary Education Curriculum* (unpublished Document).
UNICEF, (2004). *Report on Baseline Survey on Gender. Sexuality. HIV/AIDS and Life Skills in Basic Education in Tanzania Mainland.* Dar es Salaam. (Unpublished Document).

United Republic of Tanzania (URT), (2003).*Education Sector Development Plan: Primary Education Development Plan:* D*esigns for the Improvement of Quality of Primary Education.* Dar es Salaam, April 2003: MOEC (Unpublished Document)

URT, (2001).*Education Sector Development Plan: Primary Education Development Programme* (2002 -–2006), *Basic Education Development Committee (BEDC*), July 2001 (Unpublished Document)